
**TAMISEMI** yapuliza kipenga Uchaguzi Serikali za Mitaa, CHADEMA yaibua minong'ono UKURASA 3

**WAFANYABIASHARA** asali watangaziwa fursa soko China UKURASA 3



**RUSHWA YA NGONO** Wasichana viongozi watishia kuwanyima kura wabunge UKURASA 19



Wakulima na simulizi mpya ni serikalini hadi shambani

BUFE

IJUMAA AGOSTI 16, 2024 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Kilimo biashara kubadilisha maisha ya wakulima visiwani Ziwa Victoria

MLUNGULA BARABARANI

**Madereva wanasubiri utekelezaji operesheni kuweka kamera, jaketi**

•Wadai baadhi ya trafiki wamewageuza 'ATM'

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Agosti 16, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581770

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Uteuzi wa Kabudi na Lukuvi wazua jambo

**SAMIA** atoa hotuba ya dakika tatu; Wizara ya Maliasili na Utalii mfupa mgumu... *Endelea ukurasa wa 2*



William Lukuvi - **Waziri**



Prof Palamagamba Kabudi - **Waziri**



Hamza Johari - **Mwanasheria Mkuu**



Ummy Mwalimu - **Ametemwa**



Salum Hamduni - **Katibu Tawala (M)**



Angela Kairuki - **Mshauri Ikulu**

# Watumiaji wa Facebook, WhatsApp, Insta kulipwa

UKURASA 2



UKURASA WA 22

## BABA YAKE YAMAL ACHOMWA KISU

BABA yake nyota wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Lamine Yamal, mwenye umri wa miaka 17 amelazwa hospitalini...

## Profesa Janabi: Kula milo mingi ni hatari kiafya

UKURASA 7

**MICHEZO** SIMBA MAWINDONI BARA, YANGA AFRIKA UK 24

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dk Ashatu Kijaji akijadiliana jambo na Naibu Waziri wake Khamis Hamza Khamis na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Cyprian Luhemeja wakati wa kikao cha kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa zoezi la urejelezaji wa taka ngumu katika Jiji la Dar es Salaam kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumiaji mtandao Facebook kulipwa

**Na Romana Mallya**

WATENGENEZAJI maudhui wa Tanzania kupitia mtandao wa kijamii wa Facebook wenye wafuatiliaji zaidi ya 5,000 wataanza kulipwa na baadaye kufuata mtandao wa Instagram.

Meneja wa Sera za Umma META, Desmond Mushi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika warsha ya kuongeza ujuzi na uelewa unaojumuisha ujuzi sekta ya habari na majukwaa ya kidijitali nchini Tanzania.

Warsha hiyo imeandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na serikali kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) pamoja na META.

Washiriki wakiwa ni waandishi wa habari, wanafunzi wa ngazi mbalimbali za elimu, wasanii, wafanyabiashara na wadau wanaotumia majukwaa ya kidijitali ili kujipatia kipato.

Mushi alisema wameanza na mtandao wa Facebook kwa ajili ya kujifunza na ili watu waweze kulipwa ni lazima kuwapo wanaofuatilia kuhakikisha kama maudhui ni ya mtu husika.

"Tunachukua muda kuanza na Facebook ili tujifunze halafu itakuja Instagram. Watu watalipwa kwa njia nne, ya kwanza utalipwa kutokana na unachokiweka wewe na matangazo ambayo META inaweka kwenye maudhui yako.

"Mfano ukiangalia mtandao wa Youtube ukianza kuangalia unakuta kuna tangazo, kwa sababu Youtube anapata fedha inawalipa," alisema.

Mushi alitaja njia ya pili ni subscription akimaanisha kwa watakaolipwa ni kupitia mfumo wa kibiashara na watu watalipia kutazama kilichowekwa katika ukurasa wa mhusika.

"Njia ya tatu itakuwa ni ya kununua nyota kwenye ukurasa wa mhusika na hivyo fedha zinakuja kwa anayehusika.

"Njia ya nne itahusisha kampuni kutumia maudhui ya mtu binafsi aliyoweka kwenye ukurasa mfano Facebook na Instagram," alisema Mushi.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliomba jambo hilo tangu mwezi Desemba, mwaka 2021, lakini limezungumziwa sana Kenya kwa sababu Tanzania ililiomba.

"Kutokana na machafuko yaliyokuwa kule tulianza kufungua huku kabla ya Kenya. Kwa nini tulisikia Kenya na si huku, ni utashi wa serikali kutangaza kwa hiyo halikufahamika.

"Lakini hili lipo na sasa asasi mbalimbali na vyombo vya habari zimetangaza," alisema.

Mushi alisema kwa sasa kuna mambo matatu lazima yafanyike ikiwamo kufungua bidhaa na lazima mtu awe na followers (wafuatiliaji) zaidi ya 5,000 ndipo aende kuomba na kuanza kulipwa.

Alisema kigezo kingine kinachoangaliwa ni mtu kama hajapata akaunti kwa njia batili kwa sababu baadhi hununua zenye maudhui ya utupu zenye waangaliaji 5,000.

"Jambo la muhimu linaangaliwa ni akaunti inafanya nini. Hili jambo la malipo lilikuwapo na kuna baadhi ya wasanii watanzania tayari walipwa walioanzisha kampuni au akaunti zao kutokea nchi za Afrika Kusini na Dubai. Sasa hivi ukiweka akaunti ya Tanzania utalipwa, lakini zamani ilikuwa huwezi kulipwa.

Alisisitiza kwamba kwa nchi za Afrika kupitia mtandao wa Instagram hakuna nchi yenye watumiaji wenye 'followers'(wafuatiliaji) kama Tanzania.

**RAIS SAMIA AONGOZA**

"Hata kwenye viongozi wa siasa Afrika katika mtandao wa Instagram Rais Samia anaongoza.

"Tija kubwa zaidi itakuja wakati wa Instagram, lakini Facebook pia, kuna watumiaji ila matumizi na muda mwingi wengi hutumia Instagram," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Nkundwe Mwasaga, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mohammed Khamis Abdulla, alipongeza Shirika la UNESCO kwa kutoa mafunzo hayo.

Vilevile, alivikumbusha vyombo vya habari na watumiaji wa mitandao umuhimu wa kufanyia uchunguzi taarifa zilizoko mitandaoni kabla ya kuzifanyia kazi kwa sababu ndani yake zipo za kweli na za uongo.

Alisema watumiaji wa META kwa sasa wapo zaidi ya bilioni tatu na kama ingekuwa ni nchi basi ingekuwa na watu wengi.

Kadhalika, alisema maudhui ya lugha ya Kiswahili yanahitajika kwa sababu soko lake kwa sasa ni kubwa.

Pia aligusia kuhusu mradi mkubwa uliopo wa kufundisha uchumi wa kidijitali viongozi wote serikalini.

Mwakilishi Mkazi wa UNESCO Tanzania, Michael Toto, alisisitiza umuhimu wa matumizi sahihi ya mitandao.

Kadhalika, alisema matumizi ya mtandao ni lazima kufikiwa kwa umakini, huku akiahidi shirika la UNESCO lipo tayari kutoa elimu.

Mkurugenzi wa Ukuaji wa Maendeleo ya Sanaa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Edward Buganga, alimshukuru Rais Samia kwa kufungua milango ya sekta ya sanaa kupata fursa mbalimbali.

Agustino Makame, Ofisa Sanaa Mwandamizi BASATA, katika mada yake kuhusu Mfumo wa Wadau wa Sanaa (AMIS), alisema lengo lake ni kutatua changamoto za utoaji huduma kwa wasanii na wadau wa sanaa hususan huduma za usajili na utoaji vibali vya kuendesha shughuli za sanaa.

Mfanyabiashara kwa njia ya mtandao, Theresia Nyoni, alisema kupitia mkutano huo wanajifunza elimu kuhusu fursa zinazopatikana mtandaoni na kuomba serikali kutoa mafunzo kama hayo ili badala ya watu kuitumia vinginevyo iweze kuwanufaisha.

# Uteuzi wa Kabudi, Lukuvi wazua jambo

**Na Romana Mallya**

KURUDISHWA kwa Prof. Palamagamba Kabudi na William Lukuvi katika Baraza la Mawaziri kumezua jambo:

Wachambuzi wa masuala ya siasa wamesema mabadiliko yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan yaliyowarejesha wawili hao huku yakimtema Ummy Mwalimu aliyehudumu Wizara ya Afya kwa muda mrefu, yanalenga kuboresha utendaji.

Tofauti na ilivyozoeleka – kudokeza sababu za mabadiliko katika baraza la mawaziri, Rais Samia jana alitumia dakika tatu tu kuwasilisha hotuba fupi pasi na kueleza sababu za mabadiliko aliyofanya juzi usiku.

Mchambuzi wa Siasa, Abdulkarim Atiki, alisema jana kuwa kwa ujumla, mabadiliko yoyote yanayofanywa na Rais hulenga kuboresha utendaji kazi serikalini.

Alisema kurudishwa kwa Prof. Kabudi katika Wizara ya Katiba na Sheria kumechangiwa na uzoefu mkubwa alio nao katika eneo la sheria na anakidhi vigezo.

Atiki alisema anaamini kama Prof. Kabudi angekuwapo kabla ya tukio la Mbeya la kukamatwa viongozi na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), lisingefika lilikofika "kwa sababu angetumia kila aina ya njia kulitatua kutokana na uzoefu wake kisheria".

Alisema Rais Samia amefanya vizuri kwa kuwa falsafa yake ya R4 - Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reforms (Mageuzi) and Rebuilding (Kujenga upya) haziwezi kwenda kama hazitazingatiwa utu na heshima ya binadamu.

Kuhusu uteuzi wa Lukuvi kuwa Waziri Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Utaribu), Atiki alisema kiongozi huyo ni mzoefu na mkongwe, hivyo amepewa nafasi hiyo kwa kuzingatia Bunge linalokuja litakuwa ni lenye sauti nyingi kutoka chama tawala na vyama vya upinzani na si kama lililopo sasa.

"Huko nyuma alikuwapo katika wizara hii na alifanya vizuri. Na lazima tukubaliane wana-CCM, wasiokuwa na vyama au upinzani tuna mfumo wa vyama vingi na mahali pake ni bungeni," alisema.

Lukuvi na Kabudi waliondolewa katika Baraza la Mawaziri na Rais Samia Januari 8 mwaka 2022. Januari 10, 2022 wakati anaapisha wateule wapya, Rais alisema wawili hao amewavuta Ikulu ili wamsaidie kuongoza.

Kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii, alisema ina matatizo makubwa tangu zamani na ilikuwa na utulivu kidogo kipindi cha uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

"Ushauri wangu, Rais afumue mfumo mzima wa usimamizi wa rasilimali asili zote ili usimamizi wake uwe tofauti," mchambuzi huyo alisema.

Kuhusu mabadiliko yaliyohusisha Wizara ya Afya, Atiki alisema waziri kukaa zaidi ya miaka 10 si sawa, ni lazima apishe wengine kwa kuwa hizo ni nafasi za ajira.

"Vijana mpaka wanazeeka hawapati kazi na watanzania wenye uwezo wa kufanya haya mambo ni wengi hivi sasa. Kuwe na utaratibu wa kupokezana vijiti, waangalie nchi za wenzetu," alisema.

Rais Samia akizungumza wakati akiwaapisha wateule wake jana Ikulu, Dar es Salaam, aliwapongeza walioaminiwa kwa kuwaeleza kuwa mabadiliko hayo ni ya kawaida ya kuongeza ufanisi kwenye maeneo yao.

"Mmeapa viapo vinne, mkaishi na viapo hivyo na kufuata maadili ya kazi yanayotakiwa. Kama mnavyoelewa, nina vikao vya SADC (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika), sitaongea leo (jana) na ninyi ila nitawaita kwa sekta zenu siku moja moja tuzungumze kwa undani zaidi.

"Ninachotaka kusema ni kile alichosema Makamu wa Rais (Dk. Philip Mpango) kwenye utaalamu uliosomea binafsi na kujiongeza. Mtakapoona inahitajika mjiongeze tuwatumikie wananchi na tukafanye kazi," alisema Rais Samia aliyetumia dakika tatu kutoa maagizo hayo.

Awali, Dk. Mpango alisema viapo walivyokula ni vizito na kuwasihi wakaviishi katika nafasi zao walizoteuliwa.

Pia alisema matumaini ya Rais Samia na watanzania ni kwamba, watapata huduma bora kupitia nafasi hizo walizonazo.

"La sivyo watabaini kwamba tunapwaya katika nafasi zetu. Mkashirikiane na viongozi wengine mtakaowakuta katika nafasi zenu ili kwa ujumla kama taifa tuweze kwenda kwa haraka zaidi. Mwenyezi Mungu awatangulie katika nafasi zenu," alisema Dk. Mpango.

**WALIOTEULIWA**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Moses Kusikula, Mbali na Lukuvi na Prof. Kabudi, anayekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Jenista Mhagama anakuwa Waziri wa Afya baada ya Ummy aliyehudumu Baraza la Mawiziri kwa miaka 14 kuachwa.

Wengine ni Balozi Pindi Chana aliyerejeshwa Wizara ya Maliasili na Utalii, akichukua nafasi ya Angela Kairuki, aliyeteuliwa kuwa Mshauri wa Rais. Kabla ya uteuzi huu Chana alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Taarifa ya Ikulu pia ina orodha ya viongozi walioteuliwa na kuhamishwa vituo vya kazi pamoja na uteuzi wa Hamza Johari kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Johari alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) anayechukua nafasi ya Jaji Eliezer Feleshi aliyeteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, huku Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) akiteuliwa kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga.




Fundi kutoka Tanesco akirekebisha nyaya za umeme kwenye nguzo ambayo ipo ndani ya vibanda vya biashara eneo la Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwalimu apandishwa kizimbani mashtaka ya kulawiti mwanafunzi

**Halima Ikunji na Moshi Lusonzo**

MWALIMU Dotto Elias (29) wa shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Mt. Doroth iliyoko Kidatu, Manispaa ya Tabora amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Tabora, akishtakiwa kulawiti mwanafunzi wa darasa la pili ndani ya choo cha shule.

Akisoma mashtaka hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi John Mdoe, Mwanasheria wa Serikali Charles Magonza, alidai kuwa Elias alikuwa akimlawiti mtoto huyo chooni kipindi cha kunywa uji.

Alidai kuwa mnamo Julai 26, 2024, saa moja na saa mbili usiku, bibi wa mtoto huyo mwenye umri wa miaka saba, alibaini mjukuu wake amefanyiwa ulawiti huo baada ya kumkagua.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa Dotto alikana kutenda kosa la kulawiti mwanafunzi huyo. Hakimu Mdoe alisema dhamana iko wazi, lakini anapaswa kuwa na wadhamini wawili na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tano.

Licha ya dhamana kuwa wazi, mtuhumiwa alishindwa kukidhi vigezo, hivyo kupelekwa rumande mpaka Agosti 26 mwaka huu, kesi itakapoanza kusikilizwa.

**MTOTO AUAWA**

Visa vya watoto kuuawa wilayani Temeke vimezidi kuripotiwa, safari hii mwili wa mtoto wa kike anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka mitano au sita, umekutwa katika nyumba ambayo ujenzi wake haujakamilika, akiwa amebakwa na kuuawa juzi asubuhi huko Mbagala Jeshi la Wokovu, karibu na Mto Mzinga.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema jana kuwa kabla ya kuuawa, mtoto huyo alibakwa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Jeshi la Wokovu, Chauka Kikwesha, alisema mwili wa mtoto huyo uligunduliwa na wanafunzi watoro waliokwenda katika nyumba hiyo kujificha.

Kamanda Muliro alisema polisi wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ambalo ni la nne ndani ya miezi sita kuripotiwa watoto kuuawa katika mazingira ya aina hiyo wilayani Temeke.

# W'biashara asali watangaziwa fursa soko China

**Na Moshi Lusonzo**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, amesema kuwa wafanyabiashara wa asali nchini wamepata soko la uhakika nchini China, baada ya vikwazo kuondolewa.

Akizungumza katika hafla ya utiliaji saini Itifaki ya kuiuzia asali China, Waziri Kitandula, alisema mahitaji ya soko ni tani milioni 38 kwa mwaka ambayo ni fursa muhimu kwa Watanzania kuongeza uzalishaji.

Alisema wadau wa sekta ya nyuki wanatakiwa kukutana na serikali kwa ajili ya kuweka mikakati na kujipanga kuhakikisha kinapatikana kiwango kitakachokidhi mahitaji ya soko hilo jipya.

Kitandula alisema matarajio ya serikali ni kuongeza uzalishaji wa asali kutoka nchi ya pili duniani na kuwa ya kwanza kwa kufikia tani 138,000 kwa mwaka.

Alisema kwa sasa uzalishaji ni tani 33,276 sawa na asilimia 24.1 ya uwezo, kiwango kinachoifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kwa uzalishaji wa asali katika Jumuia ya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ya pili kwa Afrika na duniani inashika nafasi ya 14.

"Nawaomba wadau wa sekta ya nyuki kuhakikisha tunafikia kiwango kinachotakiwa katika soko hili kubwa, nawaomba wadau tukutane ofisini tuweke mikakati ya kupeleka bidhaa ya asali China," alisema Waziri Kitandula ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mkinga.

Alisema asali ya Tanzania huuzwa katika nchi za Ujerumani, Poland, Denmark, Uholanzi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uingereza, Marekani, Lebanon, Ubelgiji, Iraq, Saud Arabia, Kenya, Rwanda, Burundi, Congo na Uganda.

Waziri wa Mamlaka ya Forodha ya China, Yu Jianhua, ambaye alitia saini kwa niaba ya serikali yake, alisema kukamilika kwa itifaki hiyo inatokana na urafiki wa kindugu uliopo baina ya nchi hizo.

Alisema ana uhakika mamlaka za Tanzania zitajipanga kuhakikisha bidhaa hiyo inakuwa kiungo muhimu katika kudumisha kwa vitendo urafiki wa kimkakati uliobuniwa kwa serikali za nchi hizo.

Waziri Jianhua yuko nchini katika ziara inayolenga kukamilisha makubaliano yaliyofikiwa wakati Rais Samia Suluhu Hassan, alipoitembelea China, Novemba 2022.

# TAMISEMI yapuliza kipenga Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

SERIKALI imetangaza kuwa Novemba 27 mwaka huu ni siku rasmi ambayo Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika.

Vyama 18 kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu nchini vilihudhuria tukio hilo la kutangazwa tarehe ya uchaguzi huo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) hakikupeleka mwakilishi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, alitangaza tarehe rasmi ya uchaguzi huo jana jijini hapa mbele ya viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa na wadau wengine wa maendeleo.

"Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019, ibara 4 (1-3) (Matangazo ya Serikali Na. 571, 572, 573 na 574) ya mwaka 2024, ninautangazia umma wa watanzania na vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu kuwa tarehe 27 Novemba 2024 itakuwa ni siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara.

"Upigaji wa kura utaanza saa 12:00 asubuhi na kumalizika saa 10:00 jioni," alisema Mchengerwa na kueleza kuwa nafasi zitakazogombewa ni mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za wilaya.

"Kwa nafasi hizo, uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za wilaya za mwaka 2024," alisema.

Waziri huyo alisema uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za miji midogo utaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za miji midogo za mwaka 2024.

"Kwa mujibu wa kanuni hizi, ili kuwafahamisha wananchi majina ya maeneo na mipaka ambayo itahusika katika kujiandikisha na upigaji kura, wasimamizi wa uchaguzi watatangaza majina na mipaka ya vitongoji vilivyoko katika eneo la halmashauri husika siku 72 kabla ya siku ya uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji, mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa mtaa, wajumbe wa serikali ya kijiji na wajumbe wa kamati ya mtaa," alisema.

Waziri huyo alisema uteuzi wa waandikishaji na waandaaji orodha ya wapigakura kwa mujibu wa kanuni hizo, utafanywa na msimamizi wa uchaguzi atakayeteua watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa orodha ya wapigakura siku 52 kabla ya siku ya uchaguzi.

"Uandikishaji wapigakura kwa mujibu wa kanuni hizi, uandikishaji na uandaaji wa orodha ya wapigakura utaanza siku ya 47 kabla ya siku ya uchaguzi na utafanyika kwa muda wa siku 10," alisema.

"Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa kanuni hizi, mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi za uongozi, atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi husika siku zisizopungua 26 kabla ya siku ya uchaguzi kwa kadri itakavyoelekezwa na msimamizi wa uchaguzi na kutakiwa kurejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya uchukuaji fomu iliyotangazwa na msimamizi wa uchaguzi," alisema.

Waziri huyo alisema wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi watatakiwa kuwa wanachama na wadhamininiwa wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje CHADEMA, John Mrema, alipotafutwa na Nipashe jana, alisema walishindwa kushiriki tukio hilo kutokana na viongozi wakuu kuwa wagonjwa baada ya kutoka mahabusu walikoshikiliwa na polisi.

"Msajili wa Vyama vya Siasa aliandika barua ya mwaliko kwa mwenyekiti wa chama Agosti 13 mwaka huu na siku hiyo ndiyo mwenyekiti alikuwa mahabusu pamoja na makamu wake na katibu mkuu, hivyo mwaliko haukuwafikia, lakini pia walipotoka walikuwa wagonjwa kwani walikuwa wameumizwa na polisi walipokuwa mahabusu," alisema Mrema.

# HABARI KITAIFA


**THE UNITED AFRICAN UNIVERSITY OF TANZANIA**
**Plot No P9842, Vijibweni, Kigamboni Municipality**
**P.O. BOX 36246, DAR ES SALAAM, TANZANIA**
**E-mail: hr@uaut.ac.tz**

## VACANT POSITIONS

**THE UNITED AFRICAN UNIVERSITY OF TANZANIA (UAUT)** is a private university fully accredited by the Tanzania Commission for Universities. The University is located in Kigamboni, Dar Es Salaam.

**1. SENIOR LECTURER (1 POSITION)**

**(i) Qualifications**
- Holders of Ph.D. and a GPA of 3.5 (Upper Second class) or above for Bachelor degree and 4.0 or above for Master's degree majoring in Accounting, Marketing, Computer Engineering, Computer Science or related fields.
- At least 5 years of working experience in Higher Learning Institutions
- Teaching language proficiency

**(ii) Duties**
- Mentoring junior staff in all relevant areas;
- Designing and developing curricula;
- Managing institutional projects and activities;
- Writing teaching manuals and compendia and books.
- Developing new courses and programmes; and
- Undertaking any other duties that may be assigned by a relevant authority

**2. LECTURER (2 POSITIONS)**

**(iii) Qualifications**
- Holders of Ph.D. and a GPA of 3.5 (Upper Second class) or above at Bachelor degree and 4.0 or above for Master's degree majoring in Marketing, Accounting, Computer Science, Computer Engineering, IT or related fields.
- At least 3 years of working experience in Higher Learning Institutions
- Teaching language proficiency

**(iv) Duties**
- Conducting lectures, tutorials, seminars, and practical for undergraduate programmes
- Carrying out field supervision
- Mentoring junior staff in all relevant academic matters
- Participating in curriculum development
- Participating in developing and managing of various university projects
- Undertaking research and publishing research results
- Undertaking consultancy
- Preparing teaching manuals and compendia
- Supervising undergraduate students' projects
- Attending/organizing workshops, conferences and seminars

Any other relevant duties that may be assigned by the management

**3. ASSISTANT LECTURERS (2 POSITIONS)**

**(i) Qualifications**
- Holders of a Master of Accounting, Marketing, Computer Engineering, Computer Science, or related field with a minimum GPA of 4.0 and 3.5 respectively.
- Teaching language proficiency
- Graduates are highly encouraged to apply
- Working experiences in Higher Learning Institutions is an added advantage

**(ii) Duties**
- Undergoing training to PhD level
- Undergoing induction course in pedagogical skills for those who had none before
- Conducting lectures, tutorials, seminars, and practicals for undergraduate programmes
- Assisting senior staff in practical sessions, seminars, and tutorials
- Preparing case studies
- Working in cooperation with senior members on specific projects
- Supervising special projects for undergraduate students
- Mentoring junior staff in all relevant academic matters
- Participating in curriculum development
- Participating in developing and managing various university projects
- Undertaking research and publishing research results
- Preparing teaching manuals and compendia
- Attending/organizing workshops, conferences and seminars
- Any other relevant duties that may be assigned by the management

**4. HUMAN RESOURCE OFFICER**

**(i) Qualifications**

Holder of Bachelor Degree in one of the following fields; Public Administration, Human Resources Management, Industrial Relations, Business Administration/Commerce majoring in Human Resources Management or equivalent qualification from recognized institutions.

**(ii) Duties**
- Developing Recruitment Strategies to attract qualified candidates
- Design and conduct orientation sessions for new hires to familiarize them with company policies and culture.
- To develop training and development programs to enhance employee skills and performance.
- To mediate disputes between employees or between employees and management, and guide workplace issues, policies, and procedures.
- Performance Management through regular assessments.
- Compliance Management
- Payroll Management to ensure timely payment of salaries and benefits.
- Health & Safety Oversight
- Record Keeping of personnel files is essential for compliance with legal requirements, and managing data related to attendance, performance evaluations, disciplinary actions, etc.
- To interpret and implant scheme of service;
- To prepare Training Needs Assessment;
- To draft internal circulars, letters and internal memorandum for official use;
- To perform any other related duties as may be assigned by the Supervisor.

**NB:** Holders of Foreign awards certificates must have the awards verified by the Tanzania Commission for Universities (TCU) before employment.

Send your detailed CV, Cover letter, Certificates (PDF), and Testimonials (if any) to; **hr@uaut.ac.tz; and cc** nouidui@uaut.ac.tz

**This advertisement is also on our website www.uaut.ac.tz**
**Deadline 5th September 2024**




Askari wa Jeshi la Zimamoto, Polisi pamoja na wananchi mkoa wa Shinyanga wakishirikiana kuwatoa watu watatu waliopoteza maisha katika ajali ya magari mawili kugongana uso kwa uso eneo la Manzese mkoani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# ACT Wazalendo yalia na gharama matibabu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti Bara ACT Wazalendo, Isihaka Mchinjita amesema wananchi wana hofu kuhusu gharama za matibabu na ikama ndogo ya wahudumu wa afya, hivyo kuitaka serikali kutafuta ufumbuzi.

Mchinjita aliyasema hayo jana wakati anazungumza na wananchi eneo la Msanga, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya viongozi wakuu wa ACT Wazalendo iliyolenga kuyafikia majimbo 214 Tanzania Bara.

Alisema serikali inapaswa kuajiri watoa huduma ya afya wapatao 21,000 kila mwaka katika vituo vya afya ili kumaliza tatizo la uhaba huo, pia iongeze bajeti ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Mchinjita aliwataka wananchi hao kuamka na kushirikiana na ACT-Wazalendo kulinda uhuru wao, kuboresha huduma na kumaliza manyanyaso na vitisho, hasa katika umiliki wa ardhi.

Alisema huduma duni hazitoimarika kwa machozi pekee bali kwa kukiondoa Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani.

"Masuala haya yanayogusa maisha yetu ya kila siku hayawezi kuondoka kwa wingi wa machozi ya kinamama wanaokufa hospitali wakiwa wajawazito kwa kushindwa kumudu gharama za matibabu, hali hii haiwezi kuondoka kwa sababu ya vilio tulivyo navyo kwa maiti zetu zinazozuiwa hospitalini kwa kuwa tumeshindwa kuzigomboa," alisema.

Mjumbe wa Kamati Kuu ACT na Waziri Kivuli wa Utumishi na Utawala Bora, Riziki Shahari, alisema kukithiriki vitisho, ubabe na manyanyaso ya baadhi ya viongozi na watumishi kunapandikiza hofu kwa wananchi wa Pwani, hasa katika wilaya za Rufiji, Kibiti na Kisarawe.

"Tumesikia mengi kuhusu vitisho kwa watu wa Rufiji kutoka kwa watu wenye wadhifa serikalini, wananchi mna uwezo wa kumwonesha kuwa hafai kwa kuwachagua watu wengine kutoka ACT-Wazalendo," alisema.

# Morogoro yajipanga kukidhi vigezo kuwa jiji

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro, imesema inaendelea kukamilisha michakato muhimu ya kufikia vigezo vinavyotakiwa kuwa jiji.

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Mhandisi Pascal Kihanga, alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake baada ya kutoka kwenye kikao cha robo ya mwisho ya Baraza la Madiwani.

Mhandisi Kihanga alikiri katika ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan mkoani humo mwanzoni mwa mwezi Agosti, alisema hawajakidhi vigezo vya kuwa jiji, lakini wapo katika kiwango kizuri cha kufikia vigezo vinavyotakiwa na wameshaanza kukaribia vigezo vitatu vinavyohitajika vya manispaa kuwa jiji.

Ombi la kupandisha hadhi manispaa hiyo liliwasilishwa na Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood, wakati wa ziara ya kiongozi huyo.

Alivitaja vigezo hivyo kuwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato, urefu wa barabara za kiwango cha lami zilizopo na idadi ya watu kwenye eneo husika.

Alisema kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022, manispaa kuna jumla ya watu 471,000 na wanaohitajika ni 500,000, huku upungufu ukiwa ni kilometa 22 za barabara za lami ambazo wanatarajia kuzikamilisha hivi karibuni.

Alisema, ili kutimiza vigezo vya kuwa jiji na makusanyo ya mapato kwa mwaka ni Sh. bilioni 15, mwakani wanatarajia kuongeza makusanyo na kufikia Sh. bilioni 20 na kuvuka lengo la makusanyo la Sh. bilioni 17.

"Sasa kama Tanga wao ni jiji wanakusanya Sh. bilioni 17, lakini sisi mwakani tunaenda kukusanya bilioni 20, huoni kama tunaenda kuwa zaidi ya jiji," alisema Meya huyo.

Meya Kihanga aliwaomba wananchi kuwa watulivu bila kuvunjika moyo wakitambua kuwa manispaa inaendelea kutimiza vigezo na inatarajia muda mfupi ujao kuwa jiji.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akitazama chupa za dawa mbalimbali za binadamu zinazotokana na mimea dawa, alipotembelea kiwanda kidogo cha dawa hizo cha Cardenas katika Jimbo la Matanzas nchini Cuba jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mahakama yakataa ushahidi wa video kuwasilishwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Mkoa wa Dar es Salaam imekataa ombi la wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54) la kutaka shahidi Kiran Ratilal awasilishe kipande kifupi cha video (clip) kinachoonesha alivyotumbukizwa katika ndoo yenye saruji iliyokorogwa.

Nathwan na Sangita Bharat (54) wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, wanatuhumiwa kwa mashtaka manne likiwamo la kujeruhi, wanayodaiwa kuyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

Ombi hilo liliwasilishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya na Wakili wa Utetezi, Edward Chuwa kwa niaba ya wateja wake, wakati Ratilal alipokuwa akiulizwa maswali ya dodoso kutokana na ushahidi wake alioutoa dhidi ya washtakiwa hao.

Wakili Chuwa alimuuliza Ratilal ambaye ni shahidi wa nne katika kesi hiyo, kama ni kweli kwenye ushahidi wake alidai kuwa anayo 'clip' inayoonesha alivyotumbukizwa kwenye ndoo hiyo na yupo tayari kuitoa, alidai ni kweli anayo, lakini kwa wakati huo hana.

"Kwa hiyo, umeomba kuitoa mahakamani kama kielelezo kutokana na maelezo yako uliyoyatoa," alidai Wakili Chuwa.

Kutokana na madai hayo, Hakimu Lyamuya alimweleza kuwa shahidi hakuomba kutoa kipande hicho, lakini Wakili Chuwa aliendelea kudai kuwa anataka itolewe kama ushahidi.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Faraja Ngukah, alidai kuwa hawako tayari kutoa kielelezo hicho, lakini kama Chuwa anataka kufanya hivyo wanaweza kukitoa katika utetezi wao kwa kufuata utaratibu.

Wakili Chuwa alidai kuwa kama kuna hatua za kufuata yeye hazikumbuki, ndipo Hakimu Lyamuya aliwaeleza kuwa kuna taratibu za kisheria shahidi kutoa kielelezo wakati wa kipindi cha maswali ya dodoso zinatakiwa zifuatwe.

"Mahakama ya Rufaa katika uamuzi wake shauri la Lilian na Jesus ya mwaka 2018, ilitoa utaratibu, kwa hiyo Chuwa kama ulitaka kufanya hivyo ulitakiwa kufuata taratibu kwenye hiyo rufaa imeonesha hatua kwa hatua,"

"Ombi hili linakuja 'randomly' (pasi na mpangilio), ombi hili limekataliwa," alisema Hakimu Lyamuya.

Wakili Chuwa alidai kuwa wamemaliza maswali ya dodoso kwa shahidi.

Wakili Ngukah alimwuliza shahidi baadhi ya maswali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kwa mahakama, alidai upande wa utetezi ulimwuliza uhusiano wa mume wake na Hospitali ya Regency, akadai mumewe siyo daktari, ni Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo.

Wakili huyo aliiomba mahakama iwapangie tarehe ya karibu ili walete mashahidi wengine katika kesi hiyo na kudai wapo tayari kuendelea hata jana.

# TRA yatangaza siku maalumu kusikiliza kero za walipakodi

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda amesisitiza dhamira ya TRA kuendelea kuhudumia walipakodi kwa kuagiza ofisi zote za TRA mikoa yote kutenga siku ya Alhamisi kuwa mahususi kusikiliza kero na kutatua changamato za walipakodi.

Alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati akizungumza na wafanyabiashara kwa nyakati tofauti katika ziara yake inayoendelea Kanda ya Ziwa.

"Ili kuongeza ufanisi, tumekubaliana kila Alhamisi kuwa siku maalumu kwa ajili ya kusikiliza walipakodi," alisema Kamishna Mkuu Mwenda na kuongeza kuwa haimaanishi kwamba siku nyingine hawatasikilizwa, bali Alhamisi itakuwa siku maalumu, hivyo walipakodi wasisite kwenda TRA kupata huduma.

Kamishna Mkuu wa TRA pia aliwahimiza walipakodi kupakua na kuitumia app ya TRA SIKIKA ambayo aliizindua hivi karibuni, kutoa maoni, kero, ushauri na mependekezo ambayo yatamfikia moja kwa moja na atayafanyia kazi.

Baadhi ya wafanyabiashara walimpongeza na kumshukuru Kamishna Mkuu kwa kuwasikiliza na kujenga ukaribu na walipakodi, jambo ambalo wanaamini litachochea ulipaji kodi kwa hiari nchini.

Kamishna Mkuu Mwenda anaendelea na ziara kwa kutembelea, kusikiliza, kuzungumza na kutatua kero zinazowakabili walipakodi ili kujenga ukaribu na kuboresha uhusiano kati ya TRA na walipakodi na hivyo kuongeza ulipaji kodi wa hiari.

# Wakulima walalamikia wafugaji kulisha mifugo katika mashamba

**Na Agustino Kihombo,**
IRINGA

WAKULIMA wa Tarafa ya Pawaga, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, wamelalamikia vitendo vinavyofanywa na uongozi wa skimu za umwagiliaji kwa kuruhusu mifugo kuingizwa kwenye mashamba ya wakulima bila makubaliano hatua inayochochea ugomvi miongoni mwao.

Malalamiko hayo, yalitolewa na baadhi ya wakulima akiwamo Hussein Mbungu na Mgeni Kwaka katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Kinyika, Kata ya Mlenge, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa mkoani Iringa, mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James.

Kiongozi huyo alikuwa kwenye ziara katika Tarafa ya Pawaga kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo pamoja na kusikiliza kero za wananchi.

Alisema tabia inayofanywa na viongozi wao inasababisha wakulima na wafugaji kuwa kwenye migogoro kwa kuwa mifugo huingia kwenye mashamba bila makubaliano.

"Sisi malalamiko yetu ni kwa viongozi wetu wa vijiji na skimu za umwagiliaji wamekuwa wakiingia makubaliano ya kinyemela na wafugaji ya chukua hela na kuwaruhusu waingize mifugo kwenye mashamba yetu tuliyovuna mpunga, jambo hili ni kero kwa sababu wakulima hatushirikishwi juu ya maamuzi ya mashamba yetu baada ya mavuno," alisema.

Aidha, wakulima hao walilalamikia suala la mifugo kula mazao kwenye mashamba huku wakikosa msaada pindi wanapofika serikalini hali inayoongeza mashaka kwa wakulima juu ya usalama wao licha ya kuwapo kwa sheria ndogondogo za vijiji zikiainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa pindi mifugo inapoharibu mazao

"Ng'ombe wamekula mazao yangu zaidi ya ekari moja, nilipojaribu kuwatafuta viongozi sikupata majibu, nilikwenda polisi wakasema wanashughulikia mpaka leo sijapata majibu kuhusu malalamiko yangu licha ya kuwa nilipiga picha mifugo na mchungaji wake, ikiwa kwenye eneo ya shamba langu lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Hivyo, naomba Mkuu wa Wilaya utusaidie wakulima hali siyo nzuri,"alisema mkulima huyo.

Akijibu hoja hiyo, Katibu wa Skimu hiyo, Said Mohammed alisema upo utaratibu uliowekwa kupitia vikao maalumu vya kamati za wakulima zinazoelekeza namna wafugaji wanavyoweza kupata kibali cha kuingiza mifugo baada ya mavuno.

Alisema pamoja na kuwa na kibali cha serikali, muhtasari wa mkutano rasmi wa wananchi kuonesha makubaliano ya ruhusa ikiwa ni pamoja na gharama zitakazotozwa jambo ambalo halifanyiwi kazi.

"Ili mfugaji aingize mifugo yake shambani ni lazima afuate taratibu tulizojiwekea ikiwa ni pamoja na viongozi wa vijiji kuitisha mikutano na kuwaeleza wakulima uwepo wa wafugaji wanaohitaji malisho baada ya mavuno, wananchi wakiridhia unaandikwa muhtasari utakaoambatanishwa na vibali vingine vya ruhusa, lakini mfugaji kuingiza mifugo bila utatibu ni ukiukwaji wa taratibu tulizojiwekea."alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, James aliahidi kulishughulikia jambo hilo huku akihoji juu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo hilo.

Kuhusu suala la wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima, mkuu huyo wa wilaya akatoa maelekezo kwa viongozi wa vijiji vya Kata ya Mlenge, kukutana na kupata mapendekezo yatakayoamua njia bora juu ya namna wafugaji watakavyopata malisho baada ya mavuno, ili kuepusha migogoro inayotokana na viongozi hao kujitoalea maamuzi bila kushirikisha.

"Naagiza viongozi wa vijiji na jeshi la polisi kata, kuketi chini kujadili namna nzuri ya uuzaji wa mabua katika mashamba ya wakulima na gharama, ikiwa ni pamoja na kujadili matumizi ya fedha zinazotolewa, wakulima wakishindwa kuridhia mapendekezo yenu waacheni wafanye biashara wenyewe wana haki ya kufanya hivyo," alisema.

Aidha, alisema kuendelea kuruhusu wafugaji kuingiza mifugo yao kunachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazao ya wakulima kutokana na nguvu ya fedha waliyonayo jambo, ambalo ni hatari kwa usalama wa wananchi wa pande zote mbili, hivyo viongozi wanatakiwa kushirikiana na wakulima kupanga bei ita-

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu madhara ya dawa za kulevya ianzie mashuleni

**MATUMIZI** ya dawa za kulevya hasa kwa vijana yameathiri nguvu kazi na kusababisha wengi wao kuishia mitaani na kufanya vitendo vya uporaji ili wapate pesa ya kununulia dawa hizo.

Wazazi wamekuwa katika wakati mgumu hasa baada ya kujitoa kuwasomesha vijana wao na kinyume walivyotarajia kuwa watakuwa msaada, wanageuka kuwa mzigo kwa familia.

Wengi wa vijana hao wanaharibika kutokana na makundi wanayoambatana nayo na kupata vishawishi vya kutumia dawa hizo.

Baadhi ya wazazi wanatumia gharama kubwa kuwasomesha watoto wao nje ya nchi, lakini wakirudi nchini tayari wameshaathirika na madawa ya kulevya.

Kutokana na tatizo hilo, serikali imeamua kuchukua hatua ili kudhibiti kikamilifu matumizi ya dawa za kulevya nchini, kwa kupanga kuhamishia elimu inayoendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali ikiwamo kuipeleka kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu kama ilivyo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa jijini Mwanza katika kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya kupiga vita dawa za kulevya duniani alisema "ni lazima tuimarishe mikakati yetu ya kukabiliana na mapambano haya na Serikali imejikita katika kutoa elimu ili jamii ifahamu, na tutakwenda kuanzisha klabu katika shule za msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu kama walivyofanya TAKUKURU ili kupunguza kama si kumaliza kabisa tatizo hili."

Pia, vijana wa Kitanzania wametakiwa kuachana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya na badala yake waungane katika kufanya shughuli halali za kiuchumi ili wajiletee maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na hata taifa.

Kadhalika, jamii inatakiwa kuelimishwa zaidi kuhusu athari za matumizi ya dawa hizo na kuwa njia hiyo itakuwa mwarobaini wa tatizo hilo sugu pamoja na kuwawezesha waliotoka kwenye uraibu (waraibu) ili waweze kujumuika na wenzao na wafanye kazi itakayowawezesha kujisimamia.

Kuhusu taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda ya hali ya dawa za kulevya katika Mkoa wa Mwanza kuanzia mwaka 2018 hadi 2023, wananchi waliopatikana na bangi ni 1797, mirungi 294, cocaine, heroine na nyingine ni 51 na kufanya jumla ya dawa zote kuwa 2142.


Takwimu hizi zinabainisha kwamba biashara na matumizi ya dawa za kulevya mkoani Mwanza ni kubwa na inahitaji msukumo mkubwa kutoka kwa serikali pamoja na wadau mbalimbali ili kuendelea kupambana na wazalishaji, wasambaji na watumiaji wa dawa hizo.

Ukiangalia vijana wengi wanao athirika ni kutoka katika majiji ambako hufanyika mambo mengi ya starehe na hupata vishawishi vya kujiingiza kwenye matumizi hayo kama sehemu ya starehe.

Aidha, vijana wanao athirika ni wa jinsi zote na kusababisha wazazi wengine kupata msongo wa mawazo kutokana na hali wanayopitia kwani wengine hugeuka wezi kwenye nyumba zao ili wapate pesa za kuwawezesha kununua dawa hizo.

Vita ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa kwa sababu inahusisha wafanyabiashara wakubwa wenye uwezo kipesa ambao wanaweza kutumia nguvu yao ya pesa kuendeleza biashara hiyo.

Jambo la muhimu kabisa ni elimu kwa vijana hasa katika shule ambako wengi hushawishiwa kutokana na uelewa wao mdogo wa kufahamu lipi zuri na lipi baya.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# Mama,babalishe usafi ni njia kuvuna wateja

Na Sabato Kasika

**AJIRA** binafsi ndiyo habari ya mjini tena zimeshika nafasi kubwa. Watu wakijituma kufanya shughuli mbalimbali, ikiwamo biashara ya kuuza chakula au ya mama na babalishe iliyosambaa maeneo ya mijini hadi vijijini.

Hata hivyo, kundi la wauza chakula , limekuwa likikabiliwa na changamoto ya uchafu katika biashara, jambo linalohatarisha afya za wateja wao.

Baadhi yao huandaa vyakula katika mazingira ambayo si salama kwa wateja, wanasahau kwamba, kupika chakula na kukiweka katika mazingira safi, ni kuvuta wateja wakiwamo wenye pochi nene.

Hivyo, ni vyema kutambua kuwa, wakati mwingine, mamalishe wanaweza kufukuza wateja wao wenyewe kutokana na mazingira ya kuandalia vyakula kuwa machafu.

Baadhi yao huandaa vyakula katika eneo ambalo mbele kuna rundo la taka wanazozalisha, wapo inzi na wengine humwaga maji waliyooshea vyombo vya vyakula, katika mitaro iliyo karibu na eneo la biashara na kuongeza harufu mbaya kila siku.

Kuzingatia usafi katika maeneo ya biashara na kufuata kanuni za afya ikiwamo kuweka vitunzia taka, sehemu ya kuhifadhia maji na kuacha kumwaga maji machafu ovyo ni jambo la msingi.

Usafi binafsi kwa wafanyabishara wanaojihusisha na biashara ya kuuza vyakula ni moja ya mambo ya msingi ya kuzingatia ili kufanya biashara hiyo katika hali ya mvuto na afya bora.

Ikumbukwe kuwa, usafi si wa nyumbani au mwili pekee, bali hata kwenye mazingira yanayozunguka eneo la biashara, hivyo, kuanzisha biashara kama ya chakula, huku eneo la kufanyia biashara likiwa na maji machafu au uchafu wa aina yoyote, ni hatari kwake na kwa wateja.

Katika mazingira hayo, ni rahisi kukimbiwa na wateja. Ikumbukwe kuwa uchafu hukaribisha nzi, ambao husambaza magonjwa, kama vile kipindupindu na magojwa mengine ya tumbo.

Uchafu hauna faida yoyote, hivyo, wafanyabiashara hawana budi kuhakikisha wanatunza na kusafisha mazingira ya biashara zao kila siku, na kuendelea kuvutia wateja, ili wajipatie kipato cha kutosha.

Kwa kawaida ni kwamba, hakuna mteja anayejitambua ambaye anaweza kwenda kununua bidhaa fulani, katika mazingira machafu hata kama bidhaa hiyo iko karibu, badala yake atakwenda kuitafuta mbali. Hivyo, mamalishe, babalishe kumbukeni usafi ni kivutio kwa wateja.

Hivyo, sio vibaya maofisa biashara na wanaohusika na afya wakawatembelea mara kwa mara wafanyabishara na kuwaelimisha umuhimu wa kufanya biashara bila kuhatarisha afya za wateja.

Lakini pia, wafanyabiashara hao wanatakiwa kuwa na mavazi vimori au aproni na kofia, kuzingatia usafi binafsi katika wa mazingira yanayowazunguka.

Vilevile, mamalishe na babalishe, wasichukulie suala la usafi katika biashara zao kama jambo la hiari, bali kila mmoja ausimamie katika eneo lake, vinginevyo wanaweza kukimbiwa na wateja bila kujua chanzo.

Kila mfanyabiashara anayejua umuhimu wa usafi, ni vyema asaidie kuwafundisha wenzake, ili wote wauzingatie katika maeneo yao ya biashara ili wasikimbiwe na wateja na kudhani wanalogwa kumbe ni wachafu.

Inawezekana wapo baadhi yao wanaoamini kuwa kukimbiwa na wateja katika biashara zao ni kutokana na mkosi au kurogwa na kwenda kutafuta dawa kwa waganga, lakini kumbe chanzo ni wao wenyewe.

Watu wa aina ni vyema wakatambua kuwa ubunifu ni wa muhimu ili kuvutia wateja, lakini pia kuzingatia usafi ni jambo lingine lenye uzito wake katika biashara ya mamalishe na babalishe.

Ninaamini kila mmoja akiwa na kifaa cha kutunzia taka na kukitumia itakiwavyo, itakuwa rahisi kudhibiti utupaji taka ovyo kwenye eneo la biashara kama ilivyo sasa.

Lakini kikubwa zaidi ambacho kingefanyika, ni kuwatengezea maeneo ya biashara na kuwawekea miundombinu muhimu pamoja na uongozi utakaosimamia kila kitu likiwamo suala la usafi.

HABARI KITAIFA

# Ulaji wa aina hii ni hatari kwa afya

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema kundi la watu kwenye jamii linalokula milo mitano kwa siku, wanaukosesha mwili kupata muda wa kuchoma mafuta.

Profesa Janabi, ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba Shirikishi Muhimbili (MUHAS), amesema mwili wa binadamu kimaumbile hujipa majukumu kwa kujiendesha na kujirekebisha wenyewe kwa saa 24.

Katika kitabu chake: 'Mtindo wa Maisha na Afya Yako', anatoa darasa kwa umma jinsi mwili wa binadamu unavyofanya kazi na namna chakula kinavyochukuliwa, kusagwa, kutumika, kuchoma mafuta na kingine kuhifadhiwa kama akiba.

"Kimaumbile, mwili wa binadamu unajiendesha na kujirekebisha wenyewe. Jinsi chakula kinavyochukuliwa mwilini kusagwa, kutumika (fat burning) na kingine kubakia kama akiba (fat storing), hutokea wenyewe.

Kwa sababu mwili unajisimamia, binadamu anaweza tu kuratibu matumizi ya chakula mwilini kwa kuamua ale vipi, ale wakati gani na ale nini. Hali hii inatupa fursa ya kuangalia aina za kufunga ndani ya saa 24 au zaidi yaani siku tatu," anasema bingwa huyo wa magonjwa ya moyo.

Ametaja mbinu za kudhibiti milo ya mara kwa mara na mtu kupanga ratiba ya milo miwili au mmoja kwa siku, ili kutoa fursa kufanya kazi ya kujisafisha ambao kiuhalisia hutokea kwa saa 16.

"Kwa kuwa mwili unajiendesha wenyewe katika kuchukua chakula tunachokula, basi tunaweza kuudhibiti kwa kuupa chakula kwa mpangilio maalumu. Kwa maana hiyo, kama mtu ataamua kula milo miwili ndani ya saa 24, atakuwa na vipindi viwili vya kuwa na chakula tumboni ambacho huchukuliwa na kutumika.

Anasema kama mtu atapata kifungua kinywa saa sita mchana, chakula hicho huchukuliwa na kufanya kazi hadi saa tisa mchana. Baada ya hapo atakuwa katika kipindi cha kufunga, hali hiyo hulazimisha mwili kutumia akiba iliyoko.

Akiba hii inatunzwa kwenye ini, misuli au tumbo (kitambi). Hali hii ni muhimu, kwa kuwa mwili huchoma akiba hiyo ili kupata nguvu (fat burning). Hali hii huendelea mpaka pale anapokuwa amekula tena mlo wa usiku mathalani saa 12 jioni.

Baada ya mlo huo chakula huchukuliwa kwa saa tatu na hapo tumbo hubaki bila kitu. Kuanzia hapo saa tatu usiku hadi siku inayofuata saa sita mchana, mwili unakuwa na muda mrefu wa kuchukua akiba sehemu yoyote iliyopo mwilini."

Profesa Janabi anasema hatua hiyo kitaalamu ni mchakato wa mwili kujisafisha kwa kuondoa uchafu wote (autophagy) na kujenga kwa kinga imara.

Pia, iwapo mtu ataamua kula mlo mmoja pekee, ni dhahiri kwamba mwili utakuwa na muda mrefu zaidi wa kutumia akiba ya chakula kutoka sehemu yoyote ya mwili kwa kuupa nguvu.

"Kwa mfano, kama mtu atakula mlo mmoja kwa saa 24 na akala saa 12 jioni, ifikapo saa tatu usiku chakula kitakuwa kimekwisha tumboni. Baada ya hapo kuanzia saa tatu usiku, mwili utakuwa unachukua akiba kutoka sehemu mbalimbali za mwili na kuitumia.

Hali hii huupa mwili fursa ya kutumia akiba nyingi zaidi na kwa kufanya hivyo husafisha uchafu mwilini. "Kutokana na fursa hiyo tunapata manufaa ya aina mbili. Mosi, uzito hupungua zaidi au kubakia na uzito uleule; pili, kinga ya mwili hupanda kutokana na ule mchakato wa mwili kujisafisha kwa kuondoa uchafu 'autophagy' (ambao kiuhalisia unahitaji kutokea vizuri kwa saa 16 au zaidi bila kula)."

Profesa Janabu anasema kwa kipindi hicho cha mlo mmoja mtu anaweza kunywa maji au chai ya bila sukari au kitafunio muda wowote wakati wa funga hiyo, na kwamba hiyo ni aina ya ufungaji inayosababisha hali ya ukinzani wa insulini kutokuwapo kabisa, na kuepusha mtu kuingia katika hatari ya kupata kisukari.

Anatahadharisha kuwa wanaokula milo ya mara kwa mara hata kama ni kidogo, wasidhani ndio mbinu yakupunguza uzito wa mwili, kwa kuwa kufanya hivyo kunaufanya mwili kufanya kazi muda wote na kuwa na insulini. "Kwa mfano, amekunywa chai asubuhi, saa nne akala kitu kidogo, mchana akala chakula, jioni akala tena kitu na usiku akapata chakula, watu hawa hawapati muda wa kuunguza mafuta kwa wingi mwilini.

Muda wote wanakuwa na insulini mwilini ambayo inabadili wanga na sukari kuwa mafuta na kuweka akiba. Kwa kuwa mwili unalimbikiza akiba ya chakula, matokeo yake ni kuzidi kuongezeka uzito.

Wakati watu wanaokula mara kwa mara wakiongeza uzito, wale wanaofunga kwa muda mrefu wanapata faida ya kuchoma mafuta zaidi, kutoka katika akiba iliyopo mwilini na kupunguza uzito wa mwili.

"Kutokana na mtindo huo wa ulaji, jamii imejikuta ina watoto wadogo wenye uzito mkubwa na hali hiyo inakwenda mpaka kwa watu wazima. Ikumbukwe kuwa uzito uliopitiliza ni kisababishi cha magonjwa yasiyoambukiza katika umri mdogo."



Mwenyekiti wa Chama cha Tiba Asilia na Utafiti wa Mitishamba ( UMAWATI), Riziki Mkali, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu maadhimisho yao yanayotarijiwa kufanyika mkoani Pwani mwezi ujao kwa kuwakutanisha waganga wa Afrika Mashariki. **PICHA : IMANI NATHANIEL**

# TGNP yataka mifumo rafiki kwa wagombea wanawake

**Na Jenifer Gilla**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umevisisitiza vyama vya siasa kuboresha mifumo ya ndani ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu na uchaguzi mkuu Novemba mwaka 2025.

Hayo yalisemwa jana katika mafunzo kwa viongozi wa vyama vya siasa kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi na siasa, yalioandaliwa na mtandao huo.

Mafunzo hayo pamoja na mambo mengine yalilenga kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi alisema ushiriki wa wanawake katika uchaguzi unategemea mifumo ya uwezeshaji iliyomo ndani ya vyama vyao, na kuwakumbusha viongozi wa vyama vya siasa kuiboresha ili kuongeza wawakilishi wanawake.

Alitaja mifumo inayohitaji kuboreshwa kuwa ni kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi ndani ya chama kuanzia ngazi za juu hadi za chini.

"Msingi wa uongozi upo ndani ya chama, kwa hiyo kukiwa na msingi mzuri wa wanawake katika ushiriki wa ndani ya chama utawapa nguvu ya kugombea nafasi za nje," alisema.

Aliwakumbusha viongozi hao pia kuwapa elimu kuhusu kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa na namna ya kuzifikia fursa katika uchaguzi huo kwa sababu wanawake wengi wanashindwa kugombea kwa kukosa maarifa hayo.

Alisema inashangaza licha ya kuwa na idadi kubwa ya wanawake nchini uwakikishi wao katika uongozi serikali za mitaa ni asilimia 2.1 na kwamba kunahitajika mikakati ya ndani ya vyama ili kuongeza idadi hiyo.

Alisema kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 wanawake ni asilimia 51 ya Watanzania wote, ili kuiletea nchi maendeleo ni muhimu kuwapo na viongozi wa kutosha kutoka kundi hilo.

Aidha, aliwasihi viongozi wa vyama hivyo pia kutoa elimu kwa wanawake jinsi ya kuzifikia fursa zilizopo katika uchaguzi huo, ikiwamo makundi maalum na jumuishi.

"Pia, ni muhimu kuwa na wanawake wengi katika ngazi hizi za chini kwa sababu kundi hili ni walezi, wakiwa karibu na jamii ndipo tunajua mambo mengi yanayoendelea huko," alisema.

Alisema katika mafunzo hayo wanawajengea uwezo viongozi wa vyama kuhusu mambo muhimu ya kuyazingatia katika uchaguzi ili wakawaelekeze wanachama wao hasa wanawake, na kuongeza ushiriki wao katika uongozi.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Doroth Semu alishauri viongozi wa chama kukaa na wanawake katika vyama vyao na kuzungumza changamoto wanazozipitia na kuzitafutia ufumbuzi, kwa ajili ya kuwatia kushiriki uchaguzi.

Alisema kuna mazingira yanamrudisha nyuma mwanamke katika harakati za kuwania nafasi za uongozi, ikiwamo rushwa ya ngono na unyanyasaji wa kijinsia na yanapaswa kuzungumzwa kuanzia ngazi ya familia.

Aidha, alishauri wanawake kuwa uongozi ni mamlaka na hawawezi kuupata kwa urahisi ni lazima wawe tayari kukabiliana na changamoto mbalimbali wakati wanawania nafasi hizo.

Kaimu Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), Sharifa Suleiman, alisema chama hicho kimejiwekea mikakati madhubuti kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia katika uongozi ndani na nje ya chama.

Alisema kuwa, kimetunga sera ya jinsia inayoelekeza namna wanawake wanapewa fursa ya kugombea nafasi mbalimbali nchini na kutenga asilimia 20 ya bajeti yao kuliwezesha kundi hilo katika uchaguzi.

Pia, akiwa kama kiongozi upande wa Zanzibar ametembelea maeneo mbalimbali kuwapa elimu na kuwahamasisha wanawake kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kupiga kura na kugombea nafasi.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya ya Temeke wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Rashid Ngajua, alisema mafunzo hayo yamepanua akili yake ya namna ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi hasa wa serikali za mitaa.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# TANGAZO LA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2024

**Limetolewa chini ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024 (Matangazo ya Serikali Na. 571, 572, 573 na 574 ya mwaka 2024)**

**1.0 UTANGULIZI**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara 145 na 146 inaelezea uwepo wa Serikali za Mitaa pamoja na madhumuni yake. Mojawapo ya madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Aidha, Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288, zinaelekeza kufanyika kwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Lengo ni kuzifanya Serikali za Mitaa ziongozwe kidemokrasia.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 201A cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na Kifungu cha 87A cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ana mamlaka ya kutunga Kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambazo hutumika kuongoza uchaguzi huo. Viongozi wanaochaguliwa katika ngazi hizi ni wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, wenyeviti wa mitaa, wajumbe wa kamati za mitaa na wenyeviti wa vitongoji

Uchaguzi wa mwisho wa Serikali za Mitaa ulifanyika mwezi Novemba mwaka 2019, hivyo, uchaguzi mwingine unatakiwa kufanyika Novemba, 2024. Uchaguzi huu unaongozwa na Kanuni za Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya vijiji, Vitongoji na mitaa katika Mamlaka za Wilaya na Mamlaka za Miji, Matangazo ya Serikali Na. 571, 572 573 na 574 ya Mwaka 2024. Kwa mujibu wa Kanuni hizi, ninapaswa kutoa Tangazo la Uchaguzi likiainisha ratiba, shughuli za uchaguzi zinazohusika na masharti muhimu ya uchaguzi.

**2.0 MASHARTI MUHIMU YA UCHAGUZI**

Masharti muhimu ya kuzingatia katika Uchaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

**(a) Nafasi zitakazogombewa:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Nafasi zitakazogombewa katika uchaguzi huu ni:-

(i) Mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika Mamlaka za Wilaya.Kwa nafasi hizo,uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2024 (Tangazo la Serikali Na. 571 la Mwaka 2024),

(ii) Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo. Kwa nafasi hiyo, uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2024 (Tangazo la Serikali Na. 572 la Mwaka 2024)

(iii) Mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika Mamlaka za Miji. Kwa nafasi hizo, uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2024 (Tangazo la Serikali Na.573 la Mwaka 2024) na

(iv) Mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa (Kundi Mchanganyiko la Wanaume na Wanawake) na wajumbe wa kamati ya mtaa (Kundi la Wanawake) katika Mamlaka za Miji. Kwa nafasi hizo, uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2024 (Tangazo la Serikali Na. 574 la Mwaka 2024).

**(b) Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, ili kuwafahamisha wananchi majina ya maeneo na mipaka ambayo itahusika katika kujiandikisha na upigaji wa kura, wasimamizi wa uchaguzi watatangaza majina na mipaka ya vitongoji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika ***siku sabini na mbili kabla ya siku ya uchaguzi*** kwa ajili ya uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji, mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa mtaa, wajumbe wa Serikali ya Kijiji na wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

**(c) Maelekezo Kuhusu Uchaguzi:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa uchaguzi atatoa maelekezo ya ***Uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya uchaguzi.***

**(d) Uteuzi wa Waandikishaji na Waandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura:** Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura ***siku hamsini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.***

**(e) Uandikishaji wa Wapiga Kura:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya wapiga kura ***utaanza siku ya arobaini na saba kabla ya siku ya uchaguzi na utafanyika kwa muda wa siku kumi*** kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na viongozi wa vyama vya siasa.

**(f) Vituo vya Kujiandikisha, Kupiga Kura na Kupigia Kura:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, vituo vya kujiandikisha kupiga kura na kupigia kura, kwa maeneo yaliyo chini ya Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Miji Midogo vitakuwa katika ngazi ya kitongoji. Kwa upande wa Mamlaka za Miji (Miji, Manispaa na Majiji), vituo vya kujiandikisha kupiga kura na kupigia kura vitakuwa katika ngazi ya mtaa.

**(g) Muda wa Kuchukua na Kurudisha Fomu za Uteuzi:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi za uongozi, atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi husika siku zisizopungua ishirini na sita kabla ya siku ya uchaguzi kwa kadri itakavyoelekezwa na Msimamizi wa Uchaguzi na kutakiwa ***kurejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya uchukuaji wa fomu iliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi.***

**(h) Wagombea wa nafasi za uongozi:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi watatakiwa kuwa wanachama na wadhamininiwa wa Vyama vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu.

**(i) Utaratibu wa uteuzi wa wagombea:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ***husika siku kumi na tisa kabla ya tarehe ya Uchaguzi kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.***

**(j) Utaratibu wa uteuzi wa mgombea pekee:**

Endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya uenyekiti wa kijiji, kitongoji, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji, uenyekiti wa mtaa au ujumbe wa kamati ya mtaa Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi atamteua mwombaji huyo kuwa mgombea pekee kwa nafasi aliyoomba.

**(k) Pingamizi kuhusu uteuzi:**

Mgombea au mtu aliyeomba kuteuliwa anaweza kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea. Pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea litawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ***katika muda wa siku mbili tangu uamuzi au uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.***

**(l) Kamati ya Rufani:**

Kutakuwa na Kamati ya Rufani katika kila Wilaya ambayo itasikiliza pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea katika Wilaya husika. ***Wajumbe wa Kamati ya Rufani watateuliwa siku saba kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea.***

**(m) Ukomo wa kuwa Madarakani:**

Nafasi zote zinazogombewa zilikuwa na uongozi kwa kipindi cha miaka mitano. Kwa mujibu wa Kanuni hizi, viongozi hao ***watakoma kushika nafasi za uongozi siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu*** za kugombea uongozi chini ya Kanuni hizi.

**(n) Upigaji wa Kura:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, kura zitapigwa katika namna itakayozingatia usiri na kwa kutumia karatasi maalum za kupigia kura ambazo zitatakiwa kutumbukizwa katika masanduku maalum ya kupigia kura.

**(o) Waangalizi wa ndani wa uchaguzi:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi wataruhusiwa kuangalia uchaguzi baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Maombi ya kibali cha uangalizi wa uchaguzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ***ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa.***

**(p) Elimu ya Mpiga Kura:**

kwa mujibu wa Kanuni hizi, taasisi yoyote inayotaka kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi, itatakiwa kuwasilisha maombi ya kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpiga kura ulioandaliwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**(q) Kampeni za Uchaguzi:**

Kwa mujibu wa Kanuni hizi, kampeni za uchaguzi zitafanyika ***siku saba kabla ya siku ya uchaguzi***. Aidha, Kanuni zinaelekeza, kila Chama cha Siasa kinachoshiriki uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni ya uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi ***si chini ya siku saba kabla ya kuanza kwa kampeni.***

**Hivyo,** kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024 ibara 4(1-3)(Matangazo ya Serikali Na. 571, 572, 573 na 574) ya mwaka 2024, ninautangazia umma wa Watanzania na vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu kuwa tarehe **27 Novemba, 2024 itakuwa ni siku ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara. Upigaji wa kura utaanza saa mbili kamili asubuhi na kumalizika saa kumi kamili jioni.**

**Ninawatakia uchaguzi mwema, amani na utulivu katika kipindi chote cha uandikishaji, uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, wakati wa kutangaza na kupokea matokeo ya uchaguzi.**





**3.0 RATIBA YA UCHAGUZI**

Ratiba ya Uchaguzi itakuwa kama ifuatavyo:-

| NA. | TUKIO | TAREHE | MHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | Tangazo la Uchaguzi kwa Umma | 15 Agosti, 2024 | Waziri |
| 2. | Utoaji Elimu ya Mpiga Kura | 16 Agosti, 2024 | Katibu Mkuu |
| 3. | Maombi ya kuangalia uchaguzi | 30 Agosti -17 Septemba, 2024 | Katibu Mkuu |
| 4. | Tangazo la majina na mipaka ya Vijiji, Vitongoji na mitaa | 16 Septemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 5. | Uteuzi wa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo. | 19-25 Septemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 6. | Maelezo kuhusu Uchaguzi | 26 Septemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 7. | Semina kwa Wasimamizi Wasaidizi wa uchaguzi na wasimamizi wa vituo | 30 Septemba,2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 8. | Uteuzi wa waandikishaji wa wapiga kura. | 6 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi Uchaguzi |
| 9. | Viapo kwa waandikishaji wa wapiga kura, wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi | 6 - 8 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa uchaguzi |
| 10. | Elimu kwa waandikishaji wa wapiga kura | 6-8 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 11. | Zoezi la uandikishaji wa wapiga kura | 11-20 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 12. | Kubandikwa kwa Orodha ya Wapiga Kura | 21 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 13. | Ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura | 21-27 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 14. | Pingamizi kuhusu uandikishaji wa wapiga kura | 21-27 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 15. | Uamuzi kuhusu pingamizi | 27-28 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 16. | Marekebisho ya Orodha ya Wapiga Kura | 27-28 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 17. | Kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa pingamizi | 28-29 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 18. | Uamuzi wa rufaa | 28-31 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 19. | Kukoma uongozi kwa viongozi waliopo madarakani | 25 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 20. | Kuchukua fomu za kugombea | 01 Novemba, 2024 | Msimamizi Msaidizi wa |
| 21 | Kurejesha fomu za kugombea | 01-07 Novemba, 2024 | Msimamizi Msaidizi wa |
| 22. | Uteuzi wa Kamati ya Rufani | 01 Novemba, 2024 | Katibu Tawala wa |
| 23. | Semina kwa Kamati ya Rufani | 04 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 24. | Uteuzi wa wagombea | 8 Novemba, 2024 | Msimamizi Msaidizi wa |
| 25. | Uwasilishaji wa pingamizi kuhusu uteuzi | 8-9 Novemba, 2024 | Mwombaji/M gombea |
| 26. | Uamuzi wa pingamizi kuhusu uteuzi | 8-10 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 27. | Kukata rufaa dhidi ya uamuzi kuhusu pingamizi la uteuzi | 10-13 Novemba, 2024 | Mwombaji/M gombea/Msi |
| 28. | Uamuzi wa kamati ya rufaa | 10 - 13 Novemba, 2024 | Kamati ya Rufani |
| 29. | Uwasilishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni kutoka katika Vyama vya Siasa | 14 Novemba, 2024 | Vyama vya Siasa/ Msimamizi |
| 30. | Uwasilishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya | 17 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 31. | Kuanza kwa kampeni | 20 - 26 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 32. | Siku ya Uchaguzi | 27 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |

Kwa Tangazo hili, Wananchi wote wanaombwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha, kupiga kura, kugombea na kushiriki katika Uchaguzi huu ili kupata viongozi bora wa Serikali za Mitaa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mohamed O. Mchengerwa (MB.)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS**
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**

**15 Agosti, 2024**

# NBS yataka ushirikiano utafiti viashiria vya ajira

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa amewataka Watanzania wanaofikiwa na utafiti wa viashiria vya ajira nchini kutoa ushirikiano kwa makarani ili kuisaidia serikali kufanya mipango sahihi kwa kuendana na hali za wananchi.

Alitoa rai hiyo juzi jijini Mwanza wakati akikagua maendeleo ya kazi za kitakwimu na kueleza kuwa wanatarajia kuzifikia sampuli na kaya 14,500 kupata taarifa zao juu ya hali ajira ndani ya kaya.

Alisema hatua hiyo ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na Sheria ya Takwimu Sura Namba 351 inayoitaka serikali kufanya mipango kwa ajili ya wananchi kupitia takwimu zinazokidhi viwango vya kimataifa.

"Pia, sheria hii inawataka wananchi kuhakikisha mnatoa takwimu sahihi kwa makarani zinazohusu shughuli zote mnazozifanya kwa muda wa saa 24 kila siku bila kujali zipo kwenye mfumo wa ajira rasmi au shughuli binafsi," alisema Dk. Chuwa.

Ofisa Mkuu wa Ufuatiliaji wa Tathimini kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Dk. Aggrey Kinasha aliomba NBS kuhakikisha inatoa ripoti ya takwimu hizo mapema iwezekanavyo ili kuwasaidia kufanya tathmini ya matokeo ya miradi iliyopita pamoja na utekelezaji wa miradi mipya.

Alisema takwimu hizo zinakusanywa katika wilaya 10 na mikoa mitatu na kuwa itawasaidia TASAF kuandaa andiko la mradi mwingine na kutathmini utekelezaji kuendana na takwimu hizo.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala alisema wajibu wa serikali ni kuhakikisha jukumu hilo linatekelezwa kwa ukamilifu na kuwa kama viongozi wataendelea kuwahimiza wananchi kutoa takwimu sahihi katika zoezi hilo.

Diwani wa Kata ya Kiseke, Mwevi Ramadhan alisema wananchi wapo tayari na kwa maeneo ambako kazi hiyo imeanza kutekelezwa, kwamba wametoa ushirikiano wa kutosha kutokana na zoezi kuwa sehemu ya mipango ya serikali ya upatikanaji wa fursa za ajira nchini.

# Wanolewa kutathmini matokeo TPRP-IV

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WADADISI na wasimamizi wa utafiti wa kutathmini matokeo ya awamu ya nne ya mradi wa kupunguza umaskini Tanzania (TPRP-IV), wamefundwa juu ya namna ya kufanya tathmini katika mradi huo, kuja na mkakati wa kupanga mipango ya maendeleo kwa wananchi.

Akifunga mafunzo hayo juzi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ilemela, Ummy Wayayu, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kutoka kwa viongozi wa mitaa na vijiji wakati wa ukusanyaji wa taarifa, lililoanza Agosti 13 na kuendelea hadi Agosti 31 mwaka huu.

Wayayu alisema mradi huo unalenga kuboresha maisha ya kaya zinazokabiliwa na umaskini uliokithiri kwa kuziwezesha kuongeza kipato na uwezo wa kugharamia mahitaji yao muhimu.

Alisema tathmini hiyo ni muhimu ili kufahamu kama mradi unatoa manufaa kwa walengwa na jamii kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Tathmini, Ufuatiliaji, Mifumo na Mawasiliano, Japhet Boaz, alisema imepata dola za Marekani milioni 50 (Sh. bilioni 135.5) kutoka Umoja wa Nchi Wazalishaji wa Mafuta Duniani (OPEC) kwa ajili ya kutekeleza mradi huo katika mikoa ya Njombe, Arusha, Mwanza, Simiyu, na Geita ikiwa ni hatua ya kuongeza huduma za jamii na kuinua uchumi wa kaya.

Meneja wa Takwimu Mkoa wa Mwanza, Goodluck Lyimo, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwapa washiriki uwezo wa kuelewa taratibu za ukusanyaji taarifa na mbinu zinazotumika ili kupata taarifa sahihi.

Alisema: "Takwimu hizi zitatumika katika ngazi zote za utawala ili kusaidia katika kupanga mipango ya maendeleo ya wananchi na kufanya maamuzi sahihi".

# TRA, wafanyabiashara uso kwa uso kila Alhamisi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema Alhamisi ya kila wiki itakuwa ni siku maalum ya kusikiliza na kutatua kero za wafanyabiashara wote nchini.

Imesema utaratibu huo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwafikia wafanyabiashara na kutatua kero zao kuanzia ngazi za chini.

Kauli hiyo imetolewa juzi mkoani Mwanza na Mkurugenzi wa Elimu na Mawasiliano kutoka TRA, Richard Kayombo wakati akizungumza na vyombo vya habari na kueleza kuwa siku hiyo itatumika nchi nzima kuanzia kwa mameneja ngazi za Wilaya hadi Taifa.

Alisema lengo la kuanzisha siku hiyo ni kuhakikisha wanadhibiti vikwazo vyote wanavyokabiliana navyo wafanyabishara katika shughuli zao na kusababisha wasifikie malengo yao.

"Utekelezaji wa suala hili unaanza mara moja Alhamisi hii (jana), ambako kila wiki kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 11 jioni kama muda wa kazi wa siku zote bila kuathiri utaratibu mzima wa kazi wa kila siku," alisema.

Alisema siku hiyo itakuwa ikitumika kupokea malalamiko, dukuduku pamoja na maoni kutoka kwa wafanyabiashara pamoja na wananchi, hatua itakayoisaidia TRA kufikia lengo la kukusanya Sh. trilionI 30.5 kama yalivyo makadirio ya mwaka 2024/25.

Katika hatua nyingine, Kayombo alisema tayari wameandaa timu maalum kwa ajili ya kutoa elimu ya mabadiliko ya kodi yaliyotolewa Julai ili kusaidia wananchi kupata uelewa wa kila kilichobadilika.




Ukurasa 12

Wakulima na simulizi mpya ni serikalini hadi shambani



Kilimo biashara kubadilisha maisha ya wakulima visiwani Ziwa Victoria

Ukurasa 14


# BUFE

IJUMAA AGOSTI 16, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


MLUNGULA BARABARANI

# Madereva wanasubiri utekelezaji operesheni kuweka kamera, jaketi

## •Wadai baadhi ya trafiki wamewageuza `ATM'

**Na Sabato Kasika**

KATIKA moja ya hotuba zake kukemea rushwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, aliwahi kusema kuwa matrilioni ya dola yanapotezwa ili kuneemesha wachache.

Anaongeza kuwa zaidi ya asilimia tano ya pato la duniani huibwa au kulipwa kifisadi, akifananisha rushwa na shambulio kubwa zaidi la maadili duniani leo.

Anaonya kuwa ufisadi umeshamiri nchi zote bila kujali ni tajiri au maskini au ziwe kaskazini au kusini, na kwamba iwe ndogo au kubwa hupora wanajamii haki yao.

Anasema wananchi hukosa haki ya kuwa na amani kwa kuhofia kila mara kuwapa watu fulani fedha ili kupata huduma.

Pia, wanaishi kwa wasiwasi wa kuadhibiwa kama hawatatoa pesa kwa watu au kundi lenye mamlaka linalowalazimisha kufanya hivyo.

Anasema kwa taifa , rushwa inawanyima mamilioni ya maskini kujengewa shule na hospitali bora, inawapora huduma muhimu, huwapotezea muda, huleta usumbufu na zaidi ni kupora watu na mataifa rasilimali zao.

Hivi karibuni serikali imetangaza mpango wa kufunga kamera katika barabara kuu, kuondoa trafiki wengi barabarani kwani zitakapofungwa hakutakuwa na haja ya askari hao kusimamisha magari.

Ni ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan, anayefafanua kuwa kuwapo kwa kamera hizo kutakomesha rushwa inayodaiwa kufanywa na baadhi ya askari wa barabarani, kwa kuwa tatizo litakuwa limepatiwa ufumbuzi.




Moja ya majaketi yenye kifaa cha kurekodi sauti yatakayokuwa yanavaliwa na matrafiki. **PICHA: MTANDAO**

Itakumbukwa ni kauli aliyoitoa baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali akiwaambia:"Tunataka kuondoa trafiki barabarani, ili kumaliza rushwa."

Kauli hiyo ya Rais, inaonyesha wazi kuwa kuna vitendo vya rushwa vinavyofanyika barabarani ambavyo vinamkera na kuamua kukabili kwa njia ya kamera, lakini pia kwa vinasa sauti vitakavyokuwa vimefungwa kwenye majaketi wanayovaa askari hao.

Kwa mujibu wa Rais, baadhi ya askari wa usalama barabarani wanaomba rushwa, na kwamba zipo video fupi nyingi zinazowaonesha wakifanya vitendo hivyo hadharani.

Rushwa ni tatizo ambalo kama anavyosema Katibu Mkuu wa UN ni shambulio kubwa zaidi la maadili duniani.

Mhandisi wa mawasiliano ya anga na mambo ya kielektroniki, Ivan Maganza, anazungumzia juhudi hizo za kudhibiti rushwa kwenye usafiri, akisema, kamera na vifaa vya kunasa sauti, vinaweza kupunguza vitendo harakati za kupeana mlungula. Anafafanua kuwa wakati huu ni bora kwa serikali kufanya hivyo, kwa maelezo kwamba kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu mambo ya rushwa kwa baadhi ya askari wa usalama barabarani.

Anaongeza kuwa, kamera au askari anayevaa kifaa cha kurekodi, hataweza kukizima au kukiingilia akisema mfumo utamgundua.

Anaamini mtambo wa ufuatiliaji utakuwa makao makuu ya polisi au eneo jingine huria ili kufanikisha azma hiyo.

"Vifaa hivyo vinaunganishwa kwenye mtambo au ' saver', unaweza kuwekwa makao makuu ya polisi au eneo jingine serikali itakaloamua ili kufuatilia mienendo ya madereva na matrafiki," anasema Maganza.

Anaamini kuwa inakuwa si rahisi kwa trafiki aliyevaa jaketi lenye kifaa hicho kukizima, kwa kuwa wanaosimamia mtambo au 'saver' watambaini na kwamba ndiyo wenye uwezo wa kujua kila kinachoendelea.

"Lakini pia, kuna kitu kinaitwa IP, yaani 'Identity Protocol' ambayo ni namba ya utambulisho wa kifaa hicho, kwa hiyo kila aliyevaa kifaa hicho, atakuwa anajulikana pamoja na namba yake," anasema.

Anaongeza kuwa kamera na vifaa hivyo, si kwa ajili ya trafiki tu bali hata madereva na abiria, kwa kuwa vitendo vya rushwa vinahusisha pande mbili mtoaji na mpokeaji.

"Tusiwe na mtazamo kuwa kamera au vifaa hivyo ni kwa ajili ya askari tu, kwani rushwa inahusisha pande mbili, mtoaji na mpokeaji, kwa hiyo hata askari anaweza kumrekodi dereva au yeyote anayetaka kumpa rushwa barabarani," anasema. Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam na miji mingine ambayo wananchi wanalalamikia askari wa barabarani kukomalia rushwa, wanasema hatua inayochukuliwa na serikali inaweza kuwa mwarobaini wa vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya askari.

Hata hivyo wanashauri ufanyike utafiti wa kufahamu kiasi cha hasara inayopatikana kwa kutoa rushwa kwa kuwahoji madereva wa daladala na magari yakiwamo ya mikoani na malori kuujua ukubwa wa tatizo hilo.

Madereva wa daladala wanasema baadhi ya askari wanawafanya 'ATM' zao na kwamba wamezoea, na kuhofia kuwa wanaweza kuzifanyia hujuma kamera, hivyo serikali ikikamilisha kazi ya kuziweka, ifanye ufuatiliaji mara kwa mara na pia kuchunguza uharibifu na hujuma.

Wanaunga mkono kauli ya Rais Samia kuwa baadhi ya askari hao wanashiriki rushwa. Wanasema husimamisha daladala na kuwaita makondakta nyuma ya gari kisha makondakta hurudi na kuendelea na safari.

Wanahoji huko nyuma ya gari wanakutana kufanya nini, anayejua tatizo la gari ni dereva, kwa nini aende kondakta? Ndio maana tunaamini kwamba huwa kuna jambo linafanyika.

Madereva wanasisitiza kuwa polisi wanawakamua kuanzia daladala , mabasi ya mikoani, malori na pikipiki na kwamba mabilioni ya fedha yameendelea kuwafaisha watu wachache kwa miaka mingi , badala ya kujenga nchi.

Abiria wanaozungumzia mpango wa kamera na jaketi wanasema haipendezi kukuta daladala inasimamishwa muda mrefu kwa sababu ya kubishana kiasi cha fedha ambacho kondakta anatakiwa atoe ili gari iendelee na safari.

Wanasema askari hao hawajui kinachosemwa ndani ya daladala. Makondakta hawafichi wanaeleza kuwa wanawapa Sh. 1,000 au 2,000 kila wanapokamatwa yote hayo yakisababisha trafiki kudharaulika na kuonekana wazee wa kitu kidogo.

UCHUMI

NANENANE NA MBOLEA RUZUKU...

# Wakulima na simulizi mpya ni serikalini hadi shambani

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa MWANZA**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), akiangalia mbolea inayozalishwa na moja ya viwanda nchini. **PICHA: OWM.**

WAKULIMA wa mazao ya biashara na chakula wa Kanda ya Ziwa wanajivunia matumizi sahihi ya mbolea, kwani inawasaidia kupata mavuno zaidi mashambani.

Awali wengi walikuwa hawana mwamko wa kutumia mbolea kwa usahihi, sasa kumekuwapo na mageuzi, hivyo wengi wamejisajili na wananunua mbolea ya ruzuku kutoka serikalini kwa ajili ya kutumia katika msimu wa kilimo unapowadia.

Ni mchango wa Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake.Chombo kimojawapo katika kilimo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), iliyoimarishwa na kukabidhiwa jukumu la kudhibiti ubora wa mbolea nchini.

Ikajikita na jitihada ya kutoa elimu, pia kushawishi wakulima watumie mbolea iliyolengwa kwao kuwaboreshea kilimo, wakihama kutoka katika kilimo cha mazoea na sasa wanaamka kuwajibika.

Kwa Kanda ya Ziwa, wakulima wengi wanatajwa kujitokeza katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) na wanapatiwa elimu na TFRA, kuhusu matumizi sahihi ya mbolea kwenye msimu wa kilimo, huku wakiwasisitiza kujisajili ili waweze kunufaika kirahisi na mbolea ya ruzuku.

TFRA inafafanua kile ambacho, pia Nipashe ikikishushudia kwa kanda jirani, Ziwa na Kati, ambako maonesho ya Nanenane kitaifa yamefanyika mkoani Mwanza, elimu ikiendelea kutolewa kuhusu matumzi sahihi ya mbolea kwa kila msimu wa kilimo unapowadia.

### WAKULIMA WANAVYOSEMA

Zuberi Nyanda, ni mkulima wa mazao ya pamba na mahindi, anaishukuru TFRA kwa elimu, pia kisera anaishukuru serikali kwa hatua yake kuhusu usambazaji mbolea kitaifa, ikiwasaidia kwa kiasi kikubwa unafuu wa bei, unaomfanya kila mkulima kuipata.

Nyanda anasema inaonesha jinsi gani serikali ilivyowekeza katika kilimo na kupelekea wakulima kuinuka kiuchumi katika mazao wanayolima katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Kutokana na hilo, mkulima Nyanda anasema serikali isisite kuendelea kutoa mbolea za ruzuku kwa sababu zina manufaa kwao wakulima na zimechangia kwa kiasi kikubwa kuondoka katika kilimo cha

mazoea, wakihamia kulima kitaalamu kunakowapatia mavuno zaidi, tofauti na ilivyokuwa awali.

Anasema kwa msimu uliopo wakulima wengi wamenufaika na elimu iliyotolewa na

TFRA, wakulima mbalimbali wanajitokeza katika maonesho hayo ya Nanenane msimu huu kuisaka ili kunufaika.

Gabriel John anaishukuru serikali kutokana na kuleta mbolea za ruzuku kwa sababu zinawanufaisha wakulima kubadilika kutoka kwenye kilimo cha mazoea na kwenda katika kilimo cha kisasa.

Anasema awali wakulima walikuwa wanalima kiholela lakini sasa wengi wanatumia mbolea za kisasa ambazo wanapata maelekezo kutoka kwa wataalamu wa udhibiti mbolea.

Anasema kiwango cha kuvuna kimeongezeka baada ya wakulima kufuata maelekezo kutoka kwa wataalam, lakini pia kutoka kwa wataalamu wa udhibiti mbolea ambao ni mamlaka ya TFRA.

Sophia Kimaro mkazi wa Mwanza, ni mkulima anayetumia utaalamu kutoka kwa wataalam, anasema hivi sasa wengi wanalima kwa tija na wameinuka kiuchumi.

### TFRA KANDA YA ZIWA

Meneja wa TFRA Kanda ya Ziwa, Michael Sanga, anafafanua kuwa matumizi ya mbolea yamekuwa makubwa sasa, wengi wanajitokeza kununua mbolea hiyo, ikitoa ishara bora kuhusu wakulima walivyoamka kutumia mbolea.

Pia, anasifu uenezi wa serikali ya mbolea ya ruzuku, kuchangia wakulima wengi kuamka na kutumia , ilhali zamani walijikita katika kilimo cha kienyeji.

Anaongeza kuwa, leo wakulima wengi wanajitokeza kupata elimu kwa maofisa udhibiti mbolea kwenye Maonesho ya Nanenane, Kanda Ziwa.

Meneja Sanga anawashauri wakulima wasisite kufika maoneshoni na baada ya hapo katika ofisi za TFRA, wakaelimishwe maana sahihi ya mbolea ya ruzuku.

Anasema kampeni za kuelimisha matumizi ya mbolea katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na watu wameonesha uelekeo wa matumizi ya mbolea.

Sanga anasema, hivi sasa wakulima wamepata uwelewa na wengi wao wanatumia mbolea katika kilimo cha msimu kinapowadia, lakini pia wamekuwa wakiwaelimisha wenzao ambao bado hawajapata elimu sahihi ya matumizi ya mbolea shambani.

Anafafanua kuwa, wakulima wengi wanaowatembelea katika mikoa ya Kanda ya Ziwa wameonesha kuelewa matumizi sahihi ya mbolea.

Anaahidi TFRA itaendelea kutoa elimu, hata baada ya Maonesho ya Nanenane yatakuwa yamefikia ukingoni, lakini wao wataendelea kutoa elimu kwa wakulima.

Anasema hivi sasa mbolea za ruzuku zipo karibia kila sehemu na wakulima wengi wanazitumia kupanda, kukuzia na wengi wamekiri wanapata mavuno mengi tofauti na awali.

### KAULI YA SERIKALI

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akatoa pongezi kwa Wizara ya Kilimo jijini Dodoma, kutokana na maandalizi bora ya maonesho hayo kitaifa kufana, akiwataka wakulima kutumia fursa za masoko ya nje ambayo serikali inayatafuta ili kupanua wigo wa kilimo nchini, kadhalika soko la mazao yao yafike mbali nje ya Tanzania.

"Nisingependa kuona wakulima mnabaki nyuma, wakati serikali yenu ipo mstari wa mbele kuhakikisha wakulima wanapata stahiki zao, lakini pia wanapiga hatua katika kilimo wanachofanya," anasema Majaliwa.

Akawataka wakulima wadogo na wakubwa 'kuchangamkia fursa' zinazotolewa na serikali, kwa matumizi sahihi ya mbolea pamoja na vitu vingine ambavyo vipo ndani ya sekta ya kilimo.

Mwenyekiti wa Bodi ya TFRA, Dk. Anthony Diallo, anaitaka mamlaka hiyo kupitia maonesho hayo, itoe elimu kwa wakulima kuhusu kutumia mbolea katika mazao ya biashara, yatakayowainua kiuchumi katika familia.

Anataja mazao ya biashara kama pamba yazingatie utumiaji mbolea na utaalamu kutoka kwa maofisa udhibiti mbolea, pia kufuata utaalamu wa kilimo kutoka kwa

maafisa ugani.

Dk. Diallo anasema: "Serikali iko mstari wa mbele kuona wakulima wanapata mbolea na hii ndio maana TFRA inatoa elimu kwa wakulima waweze kutumia mbolea."

Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo, anasema wakulima wa mahindi wachangamkie fursa, serikali inawatafutia masoko nje ya nchi, wakajiinue kiuchumi.

Bashe anaitaja kuwa ni fursa ya ushirikiano wao na wanapaswa kujiongeza kwa kupanua wigo wa kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija kwao.

Anafafanua kuwapo kwa soko kubwa la mahindi katika nchi mbalimbali, ambazo serikali inafanya mawasiliano nazo kunahakikisha mazao ya wakulima yanauzika kimataifa.



Waziri wa Kilimo Hussein Bashe wa pili kushoto, akimkabidhi mbolea ya ruzuku aliyekuwa mkuu wa mkoa Singida, Peter Serukamba. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## TFF iunde Timu ya Taifa Kigeni, nchini, mahsusi kuipima Stars






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

TANZANIA hivi sasa ni moja ya mataifa yanayojivuna katika maendeleo ya mchezo wa soka miongoni mwa mataifa ya Afrika, ambapo inaweza kutoka kifua mbele hususan katika michuano ya klabu. kutokea kuwa taifa linalotoa timu nne kushiriki katika michuano ya kimataifa; ya Kombe la Klabu Bingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, hakika ni jambo la kujivunia sana.

Mafanikio haya yana watu nyuma yake, kwa sababu 'vinavyoelea vimeundwa', waundaji ni wachezaji, viongozi wa klabu na wadhamini chini ya usimamizi wa Shirikisho la Vyama vya Soka Tanzania (TFF) lakini kikubwa ni serikali yenyewe.

Huko nyuma tulikuwa na timu zilizoshiriki mashindano ya kimataifa, lakini hazikuwa zikifua dafu na mara nyingi zikitolewa katika mizunguko ya mapema na kubaki washangiliaji wa wenzetu.

Enzi hizo timu za Afrika Kaskazini, Magharibi na kidogo Kusini zikiogopwa sana na mataifa yetu hususan ya Afrika Mashariki, ambayo hayakuwa yakifika kokote yaliposhiriki.

Leo watu wakiitazama Tanzania wanaishangaa, kutokana na mabadiliko yaliyojitikeza ghafla, lakini pongezi zikiziendea klabu zenyewe kwa usajili mzuri, zinaoufanya kwa kuchukua wachezaji wa kimataifa, tena wanaowakilisha nchi zao kimataifa.

Klabu ya Tanzania sasa ina uwezo wa kusajili wachezaji 12 wa kimataifa kwa msimu mmoja na kuwalipa stahiki bila kukosa na hivyo kuchangia maendeleo ya mchezo huo ngazi ya klabu.

Ndiyo, TFF inaweza kutamba kuwa imechangia maendeleo ya mchezo huo, lakini kubwa ni wadhamini wenye misuli ya kutafuta wachezaji, kuwasajili na kuwalipa vizuri na kutoa mchango wao katika soka nchini.

Hata hivyo, kila mafanikio yana changamoto yake, kwani hivi sasa kinachotuangusha Watanzania ni waamuzi wetu ambapo wanachezesha si tu kwa hisia bila kufuata sheria na kanuni, lakini pia kwa kutojitambua wako katika nafasi gani na wamebeba dhamana ipi kwa Taifa. Tunashuhudia waamuzi wetu wakiachwa bila kushiriki kuchezesha mechi za kimataifa zilizoko chini ya Shirikisho la Soka la Afrika (CAF), seuze Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) Hiyo ni kutokana na uwezo mdogo walionao.

Lakini pia tunaona jinsi timu yetu ya Taifa isivyopenyeza na kushinda katika michuano mikubwa si tu ya Afrika bali hata ya dunia na kubaki kuoteotea mara moja moja, kutokana na kuwa na wachezaji wasio na uhakika.

Leo tuna timu kubwa za Ligi Kuu ya Taifa, timu zinazofanya vizuri katika michuano ya kimataifa, lakini mchango mkubwa ukitokana na wachezaji wa kigeni ambao miongoni mwao wanachezea timu zao za taifa.

TFF na serikali wamekuwa wakifanya juhudi kubwa kuhakikisha timu hii inafanya vizuri kimataifa, lakini bahati inatulalia upande wa kushoto na kushindwa kufurukuta, hata kuingia gharama za kuitafutia michezo ya kirafiki na hata hivyo kuishia kushindwa tu.Kuweka timu kambini na kuitafutia michezo ya kirafiki ili kujipima, ni jambo lenye gharama kubwa kwa raslimalifedha ya Taifa, hivyo inapofanyika hivyo na matokeo kuwa hasi, inaumiza si tu mifuko ya Taifa bali hata ya Watanzania mmoja mmoja.

Hivyo jambo la kufikiria ambalo TFF inapaswa kulifanya, ni kuzungumza na timu hizo zenye wachezaji wa kimataifa, ili kuundwa timu ya taifa ya kigeni, itakayotumika kuifanyia majaribio timu ya taifa kila kunapohitajika.

Inaeleweka wazi, kuwa hivi sasa timu za Simba, Yanga, Azam, Singida Black Stars, Coastal Union, Pamba Jiji na zingine, zina wachezaji wa kigeni wanaoweza kuunda timu moja ya kimataifa na kuifanyia majaribio Taifa Stars.

Jambo la msingi ni kuhakikisha tuna timu ya taifa ya kudumu isiwe kama inavyofanyika leo, kwamba kila yakija mashindano inatangazwa timu mpya, wachezaji wa zamani wakibaki wachache na kusababisha mifumo kutosomana.

Tukiwa na timu ya kudumu itakayokuwa inapewa wachezaji wapya linapotokea pengo, bila shaka itazoeana na mifumo kusomana na hatimaye kuwa na timu bora na imara, ikifanyiwa majaribio na Timu ya Taifa ya Kigeni, itakayoundwa na wachezaji wa kigeni walioko nchini.

Hebu TFF ikae chini ione jinsi ya kufanya na kulijaribu hili kwa maslahi mapana ya Watanzania ambao hivi sasa ni wapenzi kindakindaki wa michezo hususan soka na mingine, upenzi ulioshajihishwa zaidi na matangazo mubashara ya luninga zetu. Inshalah!

BIASHARA

# Kilimo biashara kubadilisha maisha ya wakulima visiwani Ziwa Victoria

• Kupatiwa maghala,vitalu nyumba, makaushio mazao vyote vya kisasa

**Na Beatrice Philemon**

KUTUMIA teknolojia mbalimbali kama umwagiliaji wa drip, kulima ndani ya kitalu nyumba (greenhouse), makaushio ya mazao ni utaalamu unaofanikisha kilimo biashara kinachozalisha kwa tija.

Pamoja na teknolojia hizo kilimo hicho pia kinahitaji mkulima kuwa na maghala ya kuhifadhia mazao ili kuzuia upotevu baada ya kuvuna pia vifungashio bora wakati wa kuyafikisha sokoni, anasema Philipo Mrutu.

Mrutu ni Ofisa Mtendaji wa Mrutu Agro-Solutions, kampuni inayosambaza teknolojia, elimu ya kilimo biashara na ujasiriamali, anasema kutumia na kuzingatia utaalamu na ubunifu kunafanikisha uzalishaji na kuuza mazao mengi wakati wote tena kwa faida.

**NEEMA VISIWANI**

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, Mrutu anasema ili kusaidia wakulima kujikita kwenye kilimo biashara, hivi sasa kampuni ya Mrutu Agro- Solutions, imefunga mifumo ya kitalu nyumba (greenhouse) katika kisiwa cha Chakazimbwe na Mulumo ndani ya Ziwa Victoria.

Anasema watawahudumia wakulima wanaoishi katika mazingira magumu kufanikisha kilimo cha mboga hasa nyanya, spinachi, matango na pilipili hoho.

Anasema jumla ya visiwa 10 vilivyopo ndani ya Ziwa Victoria vitajengewa mifumo ya umwagiliaji, teknolojia ya vitalu nyumba (greenhouse), makaushio ya mazao na kuwekewa maghala ya kisasa ya kuhifadhi mazao.

Anataja ujenzi wa maghala 10, vitalu nyumba10 na makaushio ya mazao 10 katika visiwa hivyo ili kuwezesha wakulima kulima kisasa, kuhifadhi na kuuza mazao kwa tija.

“Kanisa la Africa Inland Church Dayosisi ya Geita limeomba tuwasaidie watu wanaoishi kwenye mazingira magumu walime kilimo biashara kinachozingatia kanuni zote za kisasa na kiufanisi,” anasema Mrutu.

Mbali na hilo kampuni hiyo inazalisha mbegu za miche ya aina mbalimbali zinazokomaa ndani ya muda mfupi, kuzaa kwa wingi na kwa ubora kwa mfano, maparachichi, maembe, machungwa, kokoa, ndizi za aina



Mwonekano wa moja ya vitalu nyumba 10 vitakavyojengwa katika visiwa vya Ziwa Victoria kuendeleza kilimo biashara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

zote, mapera, mapapai na zikiuzwa kwa Shilingi 2,500 hadi hadi 3,000.

Anataja lengo kuwa ni kusaidia wakulima kupata mbegu bora, kujikita katika kilimo biashara chenye tija na faida, kujiongezea kipato, kupambana na umasikini na pia kuchangia pato la taifa.

Anaongeza kuwa wamesambaza miche ya mbegu 5,000 katika wilaya ya Korogwe, mkoa wa Tanga, 15,000 ya pasheni, maembe, mapera, maparachichi katika mkoa wa Dodoma, miche ya limau na maembe mkoani Mbeya.

“Tumetoa mafunzo kwa wakulima 30,000 wa Tanzania Bara na Visiwani yanayolenga kilimo biashara kazi inayofanyika kuanzia mwaka 2021 hadi sasa.”

Hadi sasa baadhi ya wakulima wameanza kulima zao la embe, vitunguu, mahindi, pilipili hoho, nyanya, matango, Chinese, bamia, nyanya chungu na wengine wameanza ufugaji wa samaki, mbuzi na uvuvi wa dagaa.

Wakati wa mafunzo wanafunzwa, ujasiriamali na kilimo biashara, kanuni na mbinu bora za uzalishaji, uchakataji, kuongeza

> **“Kuna katani kutengeneza magunia na mazulia, kamba. Shayiri kuzalisha bia na vinywaji, alizeti mafuta ya kula na zabibu kwenye mvinyo na karanga kuchakata siagi.” Anasema Mtendaji Mkuu.**

thamani, masoko na kutunza kumbukumbu za fedha.

“Kuandaa mpango wa biashara na kuwa na malengo yanayopimika, elimu ya ufugaji,fursa mbalimbali zilizopo kwenye mnyororo wa thamani kwenye kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi.” Anaongeza.

Mrutu anasema pia wanafundishwa namna ya kukabiliana na changamoto za magonjwa na wadudu waharibifu na kudhibiti upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno.

Anafafanua kuwa, wanaofanya kilimo biashara mara nyingi wanajitofautisha na wanaolima kimazoea bila faida na wanaoathiriwa na changamoto nyingi kuanzia ukame, mafuriko na visumbufu (wadudu na wanyama waharibifu kama panya na kweleakwelea).

Anataja kanuni za kilimo biashara kuwa ni kuandaa shamba mapema, kulima, kupalilia, kutumia mbegu bora, kutumia pembejeo na teknolojia kama umwagiliaji vyote kila kitu kikifanyika kwa wakati.

“Kuna kujenga miundombinu ya kilimo au ufugaji kwa kuzingatia utaalamu na nafasi, kutumia mbinu mchanganyiko ili kuzuia wadudu waharibifu na magojwa na kufanya utafiti wa soko au wateja kwanza ili kutambua changamoto na mafanikio,” anasema Mrutu.

Anataja kuongeza thamani mazao kwa kuyachakata, kutumia ubunifu ili kutofautisha bidhaa zako na za wengine, kuweka malengo na kuwa na mpango wa biashara kwa kuzingatia ubora na viwango vinavyotakiwa na mamlaka za viwango mfano TBS, TOSCI kwenye ubora wa mbegu na taasisi za usalama wa chakula na ile ya afya ya mimea na ubora na viuatilifu TPHPA.

**FAIDA KILIMO BIASHARA**

Akielezea faida za kilimo biashara, Mrutu anasema ni kuleta ajira, kwa mfano kampuni hiyo inahamasisha wakulima na wananchi kujikita kwenye kilimo biashara hasa wanawake, vijana na makundi mengine yanayonufaika kupitia mnyororo wa thamani.

“Kilimo biashara kinavipa viwanda vingi malighafi ili kutengeneza bidhaa mpya za aina mbalimbali, mfano pamba kutengeneza nguo na mazao ya nyuzi, mafuta na mashudu ya mifugo.

“Kuna katani kutengeneza magunia na mazulia, kamba. Shayiri kuzalisha bia na vinywaji, alizeti mafuta ya kula na zabibu kwenye mvinyo na karanga kuchakata siagi.” Anasema Mtendaji Mkuu.

Mbali na hilo, anasema kupitia kilimo biashara watu wanapata chakula na lishe bora ambako zaidi ya asilimia 95 ya vyakula hutokana na kilimo.

Anakumbusha kuwa, kiasi idadi ya watu inavyoongezeka na uhitaji wa chakula nao unaongezeka, hivyo hakuna budi kufanya kilimo biashara kwa tija kwa kutumia kikamilifu na kitaalamu ardhi na rasilimali nyingine zilizopo na pia kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Pia mazao na bidhaa mbalimbali zitokazo na kilimo zinapouzwa huongeza fedha za kigeni, mbali na hilo kilimo biashara kinawapatia mapato mtu mmoja mmoja na taifa.

Anasema tofauti na mtu anayefanya kilimo cha mazoea cha kujikimu, kilimo biashara lengo lake ni kujipatia faida kibiashara zaidi na kuongeza mapato.



# Vituo vya gesi asilia kuanzishwa mikoa mitatu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limesema katika mwaka huu wa fedha limepanga kuanzisha vituo vya gesi asilia mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano TPDC, Marie Msellemu alibainisha hayo juzi jijini hapa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya shirika hilo kwa mwaka huu wa fedha.

Alisema hatua hiyo itasaidia mtu kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwa kutumia gesi asilia kwa sababu ni rafiki kwa mazingira

"Vituo hivyo vitasaidia mtu kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwa usafiri unaotumia gesi asili. Usafiri huu ni mzuri na salama kwasababu hautumii gharama kubwa na ni rafiki kwa mazingira,"alisema.

Kwa upande wake Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Sophia Mwakagenda aliipongeza serikali kwa kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi.

Alisema serikali imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga vituo vya kujazia gesi asilia ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo Kwa wananchi.

Alisema: "Tuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuweka nguvu kubwa katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi na sasa serikali inaendelea kujenga vituo vya kujazia gesi hiyo ili kuwahakikisha wale wote waliobadilisha mfumo kutoka katika matumizi ya mafuta kuwa huduma ipo". kwenda sokoni kwa urahisi na kupata huduma zingine ambazo zinahitaji miundombinu mizuri ya barabara.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Exim Bank Tanzania, Jaffari Matundu, akizungumza wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 27 ya benki hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1997. Maadhimisho hayo yenye kaulimbiu 'Miaka 27 ya Kukupa Kipaumbele' yamefanyika makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wa pamba 60,000 waendesha kilimo ikolojia

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKULIMA zaidi 60,000 wa pamba katika mikoa ya Singida na Simiyu wamewezeshwa kulima kilimo cha ikolojia hai kupitia mradi wa kijani hai, chini ya Shirika la Helvetas.

Meneja wa mradi huo, Andrew Mphuru, akizungumza juzi alisema mradi wa kijani hai ulianza mwaka 2017 na mwaka huu umewafikia wakulima 60,000.

Alisema mradi huo umelenga kuwafikia wakulima 100,000 na hekta 150,00 za pamba ziwe zinalimwa kwa njia ya ikolojia hai ifikapo mwaka 2028, kwamba lengo ni kuwaondoa wakulima kuachana na kilimo cha matumizi ya kemikali.

Mphuru alisema kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya kwanza Afrika na nafasi ya tano duniani kwa uzalishaji bora na hii inachagizwa na kilimo cha pamba.

**Alisema hatua hiyo itasaidia mtu kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwa kutumia gesi asilia kwa sababu ni rafiki kwa mazingira**

Kwa upande wake Tawanda Mutonhori kutoka kampuni ya BioSustain ya mkoani Singida alisema kilimo ikolojia hai kimeweza kuongeza kiwango cha pamba bora katika mikoa ambayo wananunua.

"Sisi tunanunua pamba iliyolimwa kwa njia ya kilimo ikolojia hai kwa wakulima zaidi ya 24,000 wa mikoa ya Singida, Simiyu, na Shinyanga, kusema kweli pamba yao ni bora na inakubalika katika soko," alisema.

Alisema kwa mwaka wananunua tani 26,000 hadi 36,000 ya pamba iliyolimwa kwa njia ya kilimo hai, huku lengo lao ni kununua tani 50,000. Mwakilishi wa kampuni ya Alliance Ginery ya mkoani Simiyu, Masalu Samweli alisema kwa miaka mitatu wamewawezesha wakulima zaidi ya 22,000 kulima pamba kwa njia ya kilimo hai

Alisema walianza kutoa elimu kuhusu faida za kilimo ikolojia kiafya, kimazingira na utunzaji wa ardhi, jambo ambalo limepokelewa vizuri na wakulima hai

Alisema: "Kwa uzoefu wangu wa miaka mitatu ya kutoa elimu kuhusu kilimo ikolojia hai, uzalishaji wa mazao yasiyo na kemikali umeongezeka, hivyo wameweza kuona faida, hasa kupunguza gharama za uzalishaji".

# Mashirika ya umma yatakiwa kuzingatia sheria ya mikopo

**Na Gwamaka Alipipi**

WIZARA ya Fedha imeyataka mashirika ya umma kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Ruzuku ya Serikali, Sura ya 134 ya mwaka 2020 na kanuni zake, wakati wa kuwasilisha maombi ya mikopo ya muda mrefu wizarani kwa ajili ya kugharamia miradi mikubwa.

Wito huo umetolewa jana jijini Dar es Salaam na Kamishna Msaidizi wa Kitengo cha Usimamizi wa Madeni wa wizara hiyo, Omary Khama wakati wa utoaji mafunzo ya elimu kwa taasisi za serikali, kuhusu matakwa ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura ya 134 na miongozo mbalimbali kwenye kufadhili miradi ya maendeleo.

Alisema mashirika ya umma yana wajibu wa kuwasilisha maombi ya fedha za kufadhili miradi mikubwa inayopatikana kutoka kwa wafadhili wakubwa kama vile Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) katika wizara ili kuidhinishwa.

Khama alisema baadhi ya mashirika ya umma yamepuuza sheria inayopelekea kukopa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ambayo haina madhara yoyote kwa uchumi wa nchi.

Alisema ili kubadili mwelekeo huo, Wizara ya Fedha iliandaa mwongozo wa kupanga miradi na majadiliano ya kuongeza mikopo septemba 2020 kwa kuongeza mikopo, kutoa dhamana na kupokea ruzuku.

Alisema tangu kuidhinishwa kwa miongozo hiyo idadi kubwa ya miradi isiyo na athari yoyote ya kiuchumi ambayo ufadhili wa kukopa ilikuwa imeshuka.

Alisema kanuni zinataka miradi inayotekelezwa kwa fedha zilizokopwa lazima ionyeshe athari za moja kwa moja za kiuchumi kwa taifa na watu wake.

Alisisitiza kuwa asilimia 67 ya mikopo kutoka kwa wafadhili wakubwa hutolewa kwa riba ambayo iko chini ya asilimia moja. Wengi wao huja na kipindi cha neema ya ulipaji cha miaka 10 na zaidi ilhali muda wa kulipa hupanda hadi miaka 40.

Kadhalika alisema, Wizara ya Fedha ilitengeneza miongozo inayolenga kufikia malengo kadhaa kama vile kuongoza kwa ukamilifu hatua muhimu za mzunguko wa maisha ya mradi, mazungumzo ya ufadhili na mchakato wa kuidhinisha.

Alisema mwongozo huo unakusudiwa kuhakikisha kuwa kuna uhusiano wa wazi na usawazishaji wa shughuli kutoka kwa utayarishaji wa mradi, mchakato wa ufadhili na utekelezaji.

Alisisitiza kuwa miongozo hiyo inalenga zaidi kupunguza gharama kubwa za kukopa na tofauti za bei katika miradi yote, kwamba hutumika katika kuelezea upangaji wa mradi, uchunguzi na mchakato wa kuidhinisha.

# CCM yataka wanachama wake kutokubali kudanganywa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, kimewataka wananchi wake kutokubali kudanganywa na baadhi ya wanasiasa ambao wameanza kuwahamasisha wasiende kushiriki kupiga kura wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, alitoa wito huo jana wakati akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kijiji cha Mangida Kata ya Msange Halmashauri ya Singida Vijijini. Alisema wananchi wasiwasikilize wanasiasa wanaohamasisha wasiende kupiga kura katika uchaguzi ujao kwani kutopiga kura unakosa haki ya msingi ya kikatiba ya kumchagua kiongozi wako atakayesaidia kuleta maendeleo katika eneo lake.

"Wananchi msikubali kudanganywa na maeneo ya wanasiasa hao na badala yake jitokezeni kwa wingi kupiga kura katika maeneo yenu na muwachague viongozi ambao watasaidia kutatua changamoto zenu," alisema. Aidha, alisema serikali itaendelea kudumisha amani, utulivu na muungano wa Tanzania ili wananchi waendelee kufanya shughuli mbalimbali kwa utulivu za kujiletea maendeleo na taifa kwa ujumla.

Alisema kuna baadhi ya wanasiasa wanasema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hauna faida yoyote, akisema kwamba wanasiasa hao hawapaswi kusikilizwa wala kufuatwa maneno yao kwani hawalitakii mema taifa letu.

Mlata alisema serikali itaendelea kujenga miundombinu ya barabara ili wananchi waweze kusafirisha mazao yao kwenda sokoni kwa urahisi na kupata huduma zingine ambazo zinahitaji miundombinu mizuri ya barabara.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kutoka Mkoa wa Singida, Yohana Msita aliwataka wananchi waendelee kukiamini na kuiunga mkono CCM wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Msita alisema wananchi watumie haki yao kwa kujitokeza kwa wingi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuwachagua viongozi watakaosimamishwa na CCM kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema kupitia CCM wananchi wameendelea kupata maendeleo, kwamba serikali inatekeleza miradi mingi ya maendeleo na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Aidha, aliwataka wananchi kuacha kuwafuata wanasiasa wanaochochea chuki za ubaguzi wa ukabila, udini na ukanda kwa maslahi yao binafsi.





# Wanawake Wanging'ombe waongoza kwa kukonda

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Wilaya Wanging'ombe mkoani Njombe, inaongoza kuwa na wanawake waliokonda kwa asilimia 6.6 ikifuatiwa na Makambako yenye asilimia 5.4, huku sababu zikiwa hazijulikani.

Ofisa Lishe Mkoa wa Njombe Betha Nygu alisema hayo wakati wa wasilisho la utafiri wa hali ya lishe iliyofanyika Februari mwaka huu na kutolewa katika kikao cha tathimini ya lishe Mkoa wa Njombe, kuhudhuriwa na wananchi, wadau, viongozi wa kisiasa na serikali.

Betha alisema sababu za wanawake hao kukonda hazijajulikana na kwamba wanaendelea kufuatilia ili wabaini chanzo cha ukondefu huo .

"Halmashauri nyingine ni Makete asilimia 3.9, Njombe wilaya asilimia 3.9, Njombe mji asilimia 3.9, Ludewa asilimia 3.7," alisema Nygu.

**"Halmashauri nyingine ni Makete asilimia 3.9, Njombe wilaya asilimia 3.9, Njombe mji asilimia 3.9, Ludewa asilimia 3.7," alisema Nygu.**

Alisema kwa upande wa hali ya lishe kwa vijana balehe katika umri wa miaka 15-19 ambapo mkoa una asilimia mbili wa vijana balehe wenye uzito uliyokithiri, asilimia 15 za uzito uliyozidi na asilimia moja ya vijana balehe ambao wamekonda.

Bertha alisema katika utafiti huo pia umebaini mkoa kwa sasa una asilimia 40.2 ya watoto wenye udumavu.

Nyigu alisema mkoa umetenga bajeti ya zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa kampeni ya kutokomeza udumavu kwa kuimarisha lishe bora kwa wakazi wa mkoa huo kwa mwaka 2024/25.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alisisitiza jamii mkoani humo kuona umuhimu wa kuwa na bustani za mboga na matunda katika maeneo yao ya makazi na shule ili kuimarisha hali ya lishe.

Alisema kampeni ya kukabiliana na udumavu inapaswa kuwa endelevu kwa sababu tayari imeanza kuonyesha matokeo na watu kuwa na uelewa tofauti na kipindi cha nyuma.

Baadhi ya wakazi mjini Njombe, akiwemo Mary Sanga alisema kampeni ya udumavu iliyofanyika mkoani humo imesaidia wazazi kutambua umuhimu wa kuzingatia lishe kwa watoto wao.



Mbunge wa Mbarali mkoani Mbeya, Bahati Ndingo akisalimiana na baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Mogelo kilichopo Kata ya Rujewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali juzi alipokuwa kwenye ziara ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wakazi Mogelo walia ukosefu maji ya bomba

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wa Kijiji cha Mogelo Kata ya Rujewa wilayani Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwapelekea huduma ya maji ya bomba.

Wamesema hawajawahi kuwa na huduma hiyo hali ambayo inawalazimu kutembea umbali mrefu kwenda kuitafuta.

Walitoa malalamiko hayo wakati wa ziara ya mbunge wa Mbarali, Bahati Ndingo ambayo ilikuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua pamoja na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo.

Walisema kuwa maji wanayotumia ni machafu na yamekuwa yakiwasababishia magonjwa ya matumbo, huku wakidai kuwa wanaweza kukumbwa pia na mlipuko wa kipindupindu.

Mmoja wa wananchi hao, Juliana Lemlela alisema kutoka na yeye kuwa mzee alitakiwa awe anapata huduma hiyo jirani lakini kutokana na kutokuwepo kwa mradi wa maji ya bomba analazimika kwenda kuchota wanakochota wengine. Alisema eneo wanakochota kuna makorongo marefu hali ambayo wakati mwingine huwa inawasababishia madhara hasa kuanguka na ndoo na kuumia.

"Tatizo la maji hapa Mogelo ni kubwa sana, mimi hapa kwa umri wangu nilitakiwa nisijitwishe ndoo lakini nalazimika kujitwisha umbali mrefu, watoto wanaweza wakanisaidia lakini hawawezi kila siku maana na wao wana familia zao," alisema Juliana.

Syokhino Pailya alisema alisema kutokana na shida hiyo ya maji, wanawake na watoto huwa wanalazimika kuamka usiku kwenda kutafuta huduma hiyo kwenye makorongo hali ambayo inahatarisha maisha yao. Alisema kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani kwa eneo lao haina uhalisia kwa madai kuwa kina mama bado wanatembea umbali mrefu kufuata huduma ya maji.

Alisema mbali na wananchi wa kijiji hicho, pia wanafunzi wa Shule ya Msingi Mogelo wanatumia maji ambayo ni machafu kutoka kwenye makorongo na kwamba maji hayo wanachangia na wanyama.

"Yawezekana kupata maji ya bomba pengine ikawa gharama kubwa, sasa tunaomba serikali itusaidie tupate hata kisima, maana hali ni mbaya sana," alisema Pailya.

Aidha, mbunge Bahati alitembelea maeneo ambayo wananchi hao wanachota maji na kushuhudia hali ilivyo ambapo aliahidi kulishughulikia jambo hilo haraka kwa kuliwasilisha katika Wizara ya Maji.

Alisema katika hatua za awali za kukabiliana na tatizo hilo, atakifanyia ukarabati kisima kilichopo kijijini hapo ambacho kilichimbwa na wafadhili miaka ya nyuma ili kianze kuwahudumia wananchi wakati wakipambana kupata suluhu ya kudumu.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa wilaya ambazo zinakabiliwa na kero ya uhaba wa maji ya bomba na hivyo akasisitiza kuwa serikali iatekeleza miradi mbalimbali ya maji.

# Mil.500/- zatengwa ujenzi shule mpya Mwakibete

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kata ya Mwakibete jijini Mbeya, kutokana na ongezeko la watu linalosababisha msongamano wa wanafunzi katika shule hiyo.

Shule hiyo inatarajiwa kujengwa katika eneo la Shewa ambako mji unakua kwa kasi kutokana na serikali kuboresha miundombinu ya barabara ikiwemo Daraja la Kisasa la Dk. Tulia.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliyasema hayo juzi alipozungumza na wananchi wa Kata ya Mwakibete kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Mtaa wa Shewa ambapo alisema lengo la serikali ni kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema shule hiyo itakuwa ya mfano kutokana na kiasi cha fedha kilichotengwa kuwa kikubwa ikilinganishwa na shule zingine ambazo zimekuwa zikijengwa katika maeneo mbalimbali.

"Tumetengewa Sh. milioni 580 kwa ajili ya ujenzi wa shule hii, sasa nawaomba wananchi muendelee kutunga mkono maana serikali imefanya mambo mengi sana kwenye kata yenu," alisema Dk. Tulia.

Diwani wa Kata ya Mwakibete, Lucas Mwampiki alisema mbali na kutenga fedha hizo pia serikali imetoa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu katika Shule ya Sekondari Mwakibete ambapo wamepewa zaidi ya Sh. milioni 100. Vilevile alisema serikali inaendelea na ukarabati wa miundombinu katika Shule ya Msingi Mwakibete na Uhuru ili kuhakikisha watoto wanasomea kwenye mazingira mazuri.

"Halmashauri imeshapeleka madawati katika shule zetu zote na tunaendelea kukarabati vyumba vya madarasa ili kuhakikisha vinakuwa katika hali ambayo inaendana na hadhi ya jiji letu," alisema Mwampiki.

Alisema mbali na miundombinu ya elimu pia kata hiyo imeboreshewa miundombinu ya barabara kwa kuzijenga kwa kiwango cha lami na kuweka taa kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu.



# RC: Kuna watu wanahujumu sekta ya utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud amesema kuna baadhi ya watu wanahujumu sekta ya utalii.

Alisema hujuma hizo zinafanywa na baadhi ya vijana wanaotembeza watalii ambao hawapo kisheria na kuwasumbua wageni na kuwaibia vitu vyao vya thamani.

Alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya utalii kwa vijana wa mkoa huo ikiwa ni shamrashamra za Tamasha la Kizimkazi, mafunzo hayo yalifanyika katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Makunduchi.

Alisema kuwa, Zanzibar karibu asilimia 30 ya pato la taifa linatokana na sekta ya utalii, lakini bado sekta hiyo haijawa na thamani kwa baadhi ya watu wakiwemo vijana wanaotembeza wageni katika maeneo ya visiwa hivyo. Alisema watembeza watalii wakilalamikiwa na wageni na wawekezaji kwa kufanya vitendo viovu ambavyo havikubaliki kisheria hasa katika maeneo ya fukwe wakati wageni wakiwa wamepumzika.

**"Kumeibuka wimbi la vijana kufanya kazi ya kutembeza wageni bila ya kuwa na taaluma ya kazi hiyo jambo ambalo ni kosa kisheria" alisema Ayoub.**

Aidha alisema kuwa hali hiyo inawarudisha nyuma wawekezaji na wenye hoteli za kitalii kwa sababu wageni wanalalamika.

"Kumeibuka wimbi la vijana kufanya kazi ya kutembeza wageni bila ya kuwa na taaluma ya kazi hiyo jambo ambalo ni kosa kisheria" alisema Ayoub.

Alisema kuwa vijana waliopatiwa mafunzo hayo wanatakiwa kuwa mabalozi wazuri kwa wezao, ili kukomesha vitenda hivyo.

Hata hivyo alisema mkoa huo umejipanga kuhakikisha kuwa sekta ya utalii inapata heshima yake ili kuongeza namba ya wawekezaji wanaokwenda kuwekeza katika sekta hiyo.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Abasi Makame Muhammed, alisema kuwa sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa kwa uchumi wa Zanzibar na ndiyo maana wametoa elimu hiyo kwa vijana wanowatembeza watalii ili kuwa waaminifu.

Alisema kuwa, vijana wengi wanofanya kazi ya kutembeza wageni hawajasomea fani hiyo, ndiyo maana kukaibuka changamoto mbalimbali ikiwemo vitendo vya wizi dhidi ya wageni.



Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Ayoub akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya siku tano ya utalii yaliyo washirikisha watembeza watalii 120 kwenye ukumbi wa shule ya Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Serikali yaagiza ushirikiano kutatua tatizo la ajira

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, imezitaka taasisi mbalimbali nchini kushirikiana na kusimamia suala la ajira kwa maslahi ya taifa.

Katibu Mkuu Wizara hiyo (Kazi na Uwezeshaji), Maryam Juma Abdulla, aliyasema hayo katika kikao cha pamoja na wadau wa ajira kutoka nje ya nchi ikiwemo nchini Oman akiwemo Balozi wa Tanzania nchini humo, kilichofanyika katika ofisi za wizara hiyo Mwanakwerekwe, Zanzibar.

Alisema ushirikiano kati ya taasisi za serikali na binafsi yatatatua changamoto zinazowakabili wafanyakazi wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi, hasa katika nchi ya Oman ikiwemo masuala ya mikataba na mishahara.

Aidha, alisema kumekuwa na mgongano baina ya waajiri na waajiriwa juu ya malipo ya mishahara jambo ambalo linaloathiri ufanisi wa kazi miongoni mwa wafanyakazi.

Hivyo, aliwataka mawakala binafsi wa ajira kushirikiana na ofisi yake kuandaa mafunzo maalum kwa wafanyakazi hao kwa lengo la kuwapa uelewa juu ya namna bora ya kufanya kazi zao, kuondoa changamoto hizo na kukuza soko la ajira za ndani na nje ya nchi.

Alisema kwa utaratibu wa sasa wafanyakazi ambao wanarudi nchini kwa ajili ya likizo wanatakiwa kuwa na barua maalum kutoka ubalozi wa Tanzania ili kutambulika.

Balozi wa Tanzania nchini Oman, Fatma Mohammed Rajab, alisema Serikali ya Tanzania kupitia ubalozi wake nchini Oman utahakikisha unasimamia vyema sheria na kutetea haki za wananchi wake wanapokuwa nchini humo.

Alisema mawakala binafsi wa ajira wanatakiwa kuhakikisha kwamba wanasimamia vizuri sheria zilizowekwa ipasavyo ili kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili na ubalozi huo.

"Sisi tupo tayari kushirikiana nanyi katika mambo mbali mbali ikiwemo kuwabadilisha mawakala wasiosajiliwa kisheria ambao ndiyo sababu kuu ya changamoto zilizopo," alisema Balozi Fatma.

Alisema kwa kuwa suala la ajira ni biashara kwa sasa, hivyo aliwataka wadau hao kuhudhuria kongamano la biashara linalotarajiwa kufanyika nchini Oman kati ya Septemba 26 na 28 mwaka huu.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mawakala Binafsi wa Ajira Zanzibar, Abdul-Swamad Said Said, aliishukuru wizara, ubalozi huo na Jeshi la Uhamiaji kwa kuitisha kikao hicho ambacho kimetoa ufafanuzi juu ya masuala ambayo yanayokwamisha shughuli zao.

Pia, aliishukuru serikali kwa kuwatambua kisheria na kuwapa nafasi ya kusimamia suala la ajira za ndani na nje ya nchi.

## Waziri ataja njia mbadala kuongeza idadi ya watalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga amesema lazima kuhakikisha sekta ya michezo iende sambamba ili kuvutia watalii visiwani Zanzibar.

Alisema hayo jana katika bustani ya Forodhani Mjini Zanzibar wakati wa uzinduzi wa msimu wa nne wa mbio za riadha ambao unatarajiwa kufanyika Novemba 3 mwaka huu visiwani hapa.

Alisema vitu hivyo huwezi kuvitenganisha na Zanzibar ikitangazwa kama sehemu nzuri ya michezo ya kimataifa, kwamba itafungua milango ya aina ya watalii ambao hawajawahi kufika Zanzibar.

Soraga alisema hivi sasa kuna changamoto ya watalii wengi wanaofika Zanzibar ni wale ambao kwa ajili ya mapumziko na baadae kurejea nchini mwao, lakini wanakuwa hawana hamu ya kurejea Zanzibar kwa sababu ya kukosa shughuli za kufanya.

Aidha, alisema michezo ni sehemu nzuri sana ya kuifungua Zanzibar kuwa ni soko muhimu la michezo ambapo itasaidia kuongeza kasi ya ongezeko la watalii kupata hamu ya kurejea tena Zanzibar.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Hussein Gulam alisema mbio hizo zitawakutanisha watu mbalimbali na jambo hilo linatakiwa kuungwa mkono.

Alisema Wizara ya Elimu itaunga mkono kwa sababu ni jambo zuri la michezo ambalo litashajihisha utalii na kutimiza azma ya Rais wa Zanzibar kuwa na utalii wa michezo.

Mkurugenzi wa kampuni ya Tigo Zantel Zanzibar ambae ndiyo wadhamini wa mbio hizo, Aziz Said Ali alisema linaendeleza na kukuza utalii wa michezo.

Alisema wamekuwa wadhamini wakuu toka mwaka 2022 na ni jukwaa bora katika kukuza utalii, kukuza vibaji vya wanariadha, huimarisha afya na kuchangia katika uchumi wa buluu.

Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Riadha Zanzibar, Makame Ali Machano, alisema michezo Zanzibar ni ajira na ni Uchumi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**NELLY THOMAS MTAKI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4967-0057** kilichotolewa na **ST. ALOYSIUS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0233-0745** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. MARY'S MAZINDE JUU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/169164/2024**

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**HENRY MATHIAS LIKONDE** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba tae **319120** iliyotolewa makao makuu IDARA YA UHAMIAJI DAR ES SALAAM mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/IRI/MUF/11612/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAUDA AMINI SENDOKI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1819/0021** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TRIFONIA ACADEMY** mwaka 2011.kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/169913/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ST MARY GORET SECONDARY SCHOOL**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari Coaster yenye namba za usajili **T 416 DPS**

CHASSIS NO **HZB 300006766**

NA ENGINE NO **1HZ0080944**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi .

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/KIL/MOS/ 18620/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH FERETHA MUSHI**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T191 AAJ**

AINA YA **TOYOTA COROLLA**

,CHASISI NAMBA **AE1000137603,**

INJINI NAMBA **5AB809937** KWA YEYOTE

ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE

POLISI TAARIFA

**PHQ/DAR/KIN/171360/2024**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 19317 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: THERESIA MWINYIMVUA LIHUMBI**

**By 1: EMMANUEL ROBERT BUGANO**

**2: ________________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of 08.2024

Dated at MOROGORO this 14 day of 08.2024

RESIDENT MAGISTRAT

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT P.O.Box 660, Morogoro

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI......131......... LA 2024**

**ANETH N. PAULO..................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PATRICK LUCIANO MBEDULE.......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**PATRICK LUCIANO MBEDULE**
**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**ANETH .N. PAULO** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 5/09/2024 saa 03:00 Asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 7 Mwezi ..8..,2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA.137 YA MWAKA 2024**
**BAINA YA**
**MUSSA J KAMOTA..................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**STELLA AINEA**
**BARK ZACHARIA**
**CHRISTINA ZEBEDAYO ZEFANIA }..................WADAIWA**
**MZEE CHIUYO**
**ABUSHIRI SEIF ABUSHIRI }**
**MWANTUMU ABDALAH }**

**KWA:**
**STELLA AINEA, BARK ZACHARIA CHRISTINA ZEBEDAYO ZEFANIA, MZEE CHIUYO, MWANTUMU ABDALAH**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wew binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 19.09.2024 saa 3.00 asubuhi kwa ajili ya hukumu.
**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 02 ya Mwezi Julai 2024

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA

MWENYEKITI, Baraza la Ardhi na Nyumba

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA.179 YA MWAKA 2019**
**BAINA YA**
**NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC......................MDAI**

**DHIDI YA**

**GODFRID MICHAEL MUSHI}**
**ALFRED ANSELIM KINABO} .................................WADAIWA**

**KWA:**
**GODFFRID MICHAEL MUSHI**
**ALFRED ANSELIM KINABO**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wew binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 19.09.2024 saa 3.00 asubuhi kwa ajili ya hukumu.
**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 30 ya Mwezi Julai 2024.

MWENYEKITI, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa DAR ES SALAAM**

**Shauri la mirathi Na. 1230/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED ABEID SAID WA MZIMUNI KINONDONI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA ABDULRAHMAN MOHAMED ABEID**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)**

Watu wotw wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 4 mwezi 9 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 9 mwaka 2024

HAKIMU

---

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Madalali tajwa hapo chini kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa wadaiwa kulipa madeni yao. Baada ya hapo hatua nyingine za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na uuzwaji wa mali walizoweka dhamana ya mikopo kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Joseph Thomas Ngelela | Nyumba – Mtaa Namadoke Ilemela Mwanza | 06/09/2024 | EAGLE Recoveries LTD |
| Pili Shabanl Salum | Nyumba Na. KND029563 mtaa Mianzini-Ubungo | 30/08/2024 | King Africa General Enterprise |
| Mary-Stella Peter Temba | Gari T.924 EEX Toyota Vanguard -Tabata yard | 29/08/2024 | Waungwana Auction mart |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**EAGLE: 0767828253/0754684515**
**Waungwana: 0713 077474/0766 921429**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**
**KING AFRICA: 0687956756/0718399636**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la madai TUJIJENGE TANZANIA LTD**

**Jina la mdaiwa EVELYNE SHIJA KABELELA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**( Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa EVELYNE SHIJA KABELEGE**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**KUFIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 4 mwezi 09 Mwaka 2024 saa 3:00 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa lwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 12 mwezi 08 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 10859 OF 2024**

**In the Matter of the late ROBERT KIPIGA SOSOMA**

**And**

**In the Matter of an Application for letters of Administration by ROSE MALAIKA KACHIWILE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 19 day of 8...................... 2024

Dated at Dodoma this 18 day of 07................2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE i/c DODOMA DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 55 LA MWAKA 2023**

**HARUNA A. LUGE.......MDAI**

**DHIDI YA**

**CHIKU S. RAMADHANI..........MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

UNAJULISHWA KWAMBA SHAURI TAJWA HAPO JUU LIMEPANGWA KUSIKILIZWA NA MAHAKAMA HII TAREHE 22/08/2024 SAA TATU (3:00) ASUBUHI MBELE YA MHE. E. E. KAKOLAKI, UNATAKIWA KUHUDHURIA WEWE BINAFSI AU WAKILI WAKO KISHERIA.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO KWA TAREHE TAJWA, KESI HII ITAENDELEA KUSIKILIZWA BILA WEWE KUWEPO MAHAKAMANI NA KUTOLEWA MAAMUZI.

HATI HII IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 24/07/2024

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MPWAPWA**

**LILILOKO MPWAPWA**

**MAOMBI MADOGO NA. 03 YA MWAKA 2024**

**DAUDI YOHANA CHILONGANI................................ MDAI**
**VERSUS**
**MELLY MANENO.................................... MDAIWA**

**KWA:**
**MELLY MANENO**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 15.10.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 ya mwezi wa JULY, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
MPWAPWA.

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa*

*Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie, 0677 020701*

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUDA EDMUND SOKA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **KLUGER** yenye usajili namba **T 596 DGS,** CHASSIS NAMBA: **ACU250018452** na ENGINE NAMBA : **2AZ0887705.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/171820/2024**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 264 LA 2024**

**JANETH PAUL RAPHAEL & 4 OTHERS... MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ALLY MJINGA KALIME................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**ALLY MJINGA KALIME, POPOTE ULIPO/MLIPO**

**JANETH PAUL RAPHAEL & 4 OTHERS** Amefungua/wamefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na Nyumba lililopo kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 23/9/2024 saa 03:00 asubuhi mbele ya **Mh. J.W. SILLAS** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini ya MHuri wa Baraza hili leo tarehe 13 Mwezi 08 ..,2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA / KITAIFA

# Uingereza yaruhusu Ukraine kutumia silaha zake Russia

**LONDON, Uingereza**

UINGEREZA imeiruhusu Ukraine kutumia silaha zake katika ardhi ya Russia wakati wa kujilinda.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi, alisema Ukraine ina haki ya wazi ya kujilinda dhidi ya mashambulizi ya Russia na hilo haliondoi matumizi ya silaha zilizotoka nchini humo ndani ya Russia.

„Tunaweka wazi wakati tunawapa vifaa kwamba vitatumika kulingana na sheria za kimataifa," alisema

Ben Wallace, ambaye ni waziri wa zamani wa ulinzi kutoka chama cha Conservative, aliripotiwa awali akieleza kwamba silaha zote zinazotolewa na Uingereza, isipokuwa makombora ya masafa marefu ya Storm Shadow, zinaweza kutumika ndani ya Russia.

Wakati kauli hiyo ikitolewa, tayari kumeripotiwa kuonekana kwa silaha zilizotolewa na nchi za Magharibi zikiwa ndani ya Russia, tangu Ukraine ilipoanzisha mashambulizi yake mapya mapema mwezi huu.

Zana hizo ni pamoja na magari ya kivita ya Bradley na Stryker yanayotolewa na Marekani pamoja na Marders yaliyotolewa na Ujerumani.

Hata hivyo, hakuna picha zinazoonyesha kuwepo kwa mizinga ya Challenger ya Uingereza au ya Abrams kutoka Marekani kwenye eneo la mpakani.

Hata hivyo, wataalamu wa kijeshi wa nchi za Magharibi wameelezea mafanikio ya mashambulizi ya Ukraine yanatokana na kutumia vizuri askari, magari ya kivita, mizinga,vifaru na ndege zisizo na rubani kushambulia. Hali hiyo haikuwepo katika shambulio la mwaka jana katika eneo la kusini na mashariki mwa nchi hiyo, ambalo lilizuiliwa na ngome za Russia.

Moja ya mizinga 14 ya Uingereza iliyopewa Challenger 2 iliharibiwa katika shambulio hilo lililozuiwa.

Vifaru vya Uingereza vilivyotolewa msaada vimekuwa vikiendeshwa na kikosi cha 82 cha mashambulizi ya anga cha Ukraine, ambao walipata mafunzo kwa mara ya kwanza nchini Uingereza jinsi ya kutumia Challenger 2.

Imeelezwa kuwa Ukraine imetumia baadhi ya vitengo vyake vilivyofunzwa na kuwa na vifaa bora kufanya mashambulizi yake ya kuvuka mpaka.

***BBC***



Wapalestina wakishuhudia uharibifu baada ya mashambulizi ya Israel katika makazi yao eneo la Gaza juzi. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Wasichana viongozi watishia kuwanyima kura wabunge

**Na Elizabeth Zaya**

WASICHANA viongozi wanaowakilisha kundi la vijana, wamesema wako tayari kuadhibu wabunge katika uchaguzi ujao kwa kutowapigia kura endapo watapitisha mabadiliko yaliyoainishwa katika kifungu cha 10(b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Ngono.

Wasichana hao wamesema kifungu hicho hakifai kwa kuwa kinamhukumu mwathirika wa rushwa ya ngono, kuhalalisha na kuendeleza matumizi mabaya ya mamlaka au baadhi ya watu kutumia mamlaka yao vibaya kuomba rushwa ya ngono.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana wasichana hao walisema kifungu hicho kinapaswa kufutwa kwa sababu kinakwenda kinyume na dhana ya kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Kadhalika, walisema kifungu hicho kinalenga kumlinda mhalifu badala ya kuwa msingi wa kuzuia uhalifu na kulinda haki.

"Sisi viongozi wanawake vijana, tunadai kifungu cha 25 kibaki kama kilivyo na kiendelee kutumika kwa kuwa kinajitosheleza bila kumbagua mhalifu awe wa kike au wa kiume," alisema Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kutoka Shirika la Msichana Initiative, Sara Bedah.

Kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa namba 11 ya mwaka 2007, rushwa ya ngono imetafsiriwa kuwa mtu yeyote mwenye mamlaka katika kutekeleza majukumu yake, anadai au anaweka sharti la ngono, upendeleo mwingine wowote kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au upendeleo wowote unaotambulika kisheria atakuwa ametenda kosa. Sehemu ya kifungu hicho cha 10(b) ambacho wasichana hao wananataka kifutwe inaeleza kwamba; "Kuahidi, kutoa au kutoa upendeleo wa kingono au upendeleo mwingine wowote kwa mtu ambaye yuko katika nafasi ya madaraka au mamlaka, kumshawishi kutumia mamlaka yake kwa niaba yake katika kumpa ajira, kumpandisha cheo, haki, heshima au matibabu ya upendeleo mwingine, anatenda kosa."

"Na baada ya kutiwa hatiani atawajibika kwa kulipa faini ya si chini ya Sh. milioni mbili, lakini isiyozidi Sh. milioni 10 au kifungo cha muda wa si chini ya miaka mitano, lakini kisichozidi miaka 10 au vyote viwili."

Sara alisema kilio cha wasichana hao ni kuliomba bunge lisipitishe au kukubali mabadiliko ya kifungu hicho.

"Na endapo bunge litapuuza madai yetu na sisi hatutokuwa tayari kuwapigia kura katika uchaguzi ujao na wafahamu kabisa kwamba sisi vijana ndio kundi kubwa zaidi na wapiga kura," alisema Sara.

"Endapo bunge litapuuza madai yetu, tunamuomba Rais Samia asiridhie mabadiliko hayo atakapopelekewa na bunge kwa ajili ya kusaini kwa kuwa athari zake ni kubwa kwa taifa," alisema Sara.

Hellen Sisya, alisema suala la rushwa ya ngono linawaathiri zaidi wasichana na kwamba hawatanyamaza kupiga kilele kufutwa kwa kifungu hicho cha 10(b). "Kama wanawake vijana viongozi, tumeona hatuwezi kunyamaza kuhusu hili kwa sababu suala la rushwa ya ngono linatuathiri sisi kwa kiasi kikubwa nyumbani, vyuoni, kazini, kwenye sanaa, michezo, kwenye biashara na hata eneo la siasa," alibainisha Hellen.

"Lakini tunashangazwa na kuendelea kupuuzwa kwa mapendekezo ya wadau mbalimbali ya kutaka kufutwa kwa kifungu hiki cha 10(b) kinachohalalisha na kuendeleza matumizi mabaya ya mamlaka kwa njia ya kumhukumu mwathirika wa rushwa ya ngono, tunaona hii ni mbinu ya kuwanyamazisha na kuzima moto wa mapambano dhidi ya rushwa ya ngono," aliongeza.

## Benki Exim yaadhimisha miaka 27 ya huduma kwa Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imeadhimisha miaka 27 tangu kuanzishwa kwake katika safari inayoitaja imejaa mafanikio, ubunifu na huduma bora kwa wateja wake.

Maadhimisho hayo yanafanyika chini ya kaulimbiu ya 'Miaka 27 ya Kukupa Kipaumbele', ikiangazia mafanikio yake na mikakati madhubuti ambayo imejiwekea ili kuendeleza mafanikio hayo miaka mingi ijayo.

Akizungumza wakati hafla hiyo iliyofanyika jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu, alieleza baadhi ya mafanikio makubwa ambayo benki imefikia tangu kuanzishwa mwaka 1997.

„Miaka 27 iliyopita, tulianza safari ya kubadilisha sekta ya benki nchini na leo tunajivunia kuwa miongoni mwa watoahuduma bora wa kifedha. Mpaka sasa tumevuka mipaka tukiwa na matawi katika nchi tatu za Comoro, Djibouti na Uganda," alisema.

Kwa mujibu wa Matundu, dhamira ya benki hiyo ya ubunifu imekuwa nguzo kubwa katika mafanikio yake, akitolea mfano tuzo iliyotunikiwa ya ‚Chapa ya Benki Yenye Ubunifu Mkubwa Tanzania – 2024' inayotolewa na jarida maarufu duniani la International Business Magazine.

Matundu alisema hatua hiyo ni ushahidi wa huduma bora zinazotolewa na benki hiyo.

„Uboreshaji wa hivi karibuni wa mfumo wake wa Kibenki (CBS) ni sehemu ya mikakati ya Exim Bank kuboresha na kuongeza uharaka wa miamala, usahihi na huduma bora kwa wateja kiujumla," alisema.

Matundu alisema kuwa mwaka 2023, Benki ya Exim ilipata mafanikio makubwa ya kifedha, ikiwa na faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 91.5, uwekaji wa fedha za wateja kufikia Sh. trilioni 2.4 na jumla ya mali ikivuka Sh. trilioni tatu.

„Mafanikio haya yanaonesha kiwango cha uaminifu wa Benki ya Exim kwa wafanyakazi na imani kwa wateja wake. Tutaendelea kukua na kujipambanua zaidi kuongeza wigo na kufikia maeneo zaidi ndani na nje ya Tanzania.

„Tutaendelea kuwa wabunifu, kutafuta namna bora zaidi za kutoa huduma kwa wateja wetu na hivyo kuchangia katika maendeleo ya sekta ya kifedha.

„Tuna malengo ya kuboresha ufanisi wa utendaji wetu, huduma kwa wateja na bidhaa tunazotoa kuhakikisha Exim Bank inaendelea kuwa kinara katika sekta ya kibenki nchini," alisema.

HABARI MICHEZO

# ADEBAYOR AWASILI NCHINI KUIBEBA SINGIDA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE winga wa kimataifa ya Niger, Victorien Adebayor, amewasili nchini kwa ajili ya kujiunga na Singida Black Stars inayojiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza, amesema jana mchezaji huyo amewasili na kuondoa wasiwasi kwa mashabiki wao ambao walikuwa hawaamini kama nyota huyo anaweza kutua nchini.

„Siku ya Singida Big Day ni moja kati ya wachezaji tuliowatambulisha ingawa hawakuwepo uwanjani ni Adebayor na Ibrahim Rashid Parapanda, kwa bahati nzuri, Adebayor amewasili na hivi punde atajiunga na timu kwa upande wa Parapanda yeye siku chache zijazo tunatarajia atajaunga na sisi," alisema Massanza.

Mchezaji huyo raia wa Niger amejiunga na timu hiyo akitokea GNN ya nchini kwao baada ya kumalizana na AmaZulu ya Afrika Kusini.

Mwaka 2020, winga huyo alitakiwa kwa udi na uvumba na Wekundu wa Msimbazi, akiwa katika klabu ya USGN ya Niger baada ya kufanya vizuri katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini aliwahiwa na RS Berkane ya Morocco na baada ya hapo viongozi wa Simba hawakuwa tena na habari naye, licha alikuwa kipenzi cha mashabiki wa timu hiyo wakitaka asajiliwe.

Alikuwa mfungaji bora katika michuano ya Kombe la ShirikishoAfrika mwaka juzi, na kuzivutia klabu nyingi kiasi cha kupanda dau kubwa lililoishinda Simba.

Wakati huo huo, kikosi cha Singida Black Stars kimeondoka mkoani humo kuelekea jijini Mbeya kwa ajili ya kucheza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu dhidi ya Ken-Gold.

Massanza alisema kikosi cha wachezaji 23, benchi la ufundi viongozi kimeelekea Mbeya tayari kutupa karata katika mechi yao ya kwanza itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

"Tunakwenda kupambana kuhakikisha tunapata ushindi katika mechi yetu ya kwanza kwa sababu ni muhimu sana," alisema ofisa huyo.



Magolikipa wa Timu ya Taifa ya Wasichana chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti Girls), wakijifua kwa ajili ya kwenda kushiriki mashindano ya Ukanda wa UNAF yatakayofanyika nchini Tunisia hivi karibuni. **PICHA: TFF**

# Shawwal kushiriki Paralimpiki

**Na Enock Charles**

MTANZANIA, Hilmy Shawwal (27) ambaye anaishi Uingereza ndiye mwakilishi pekee wa nchi aliyepata nafasi ya kushiriki mashindano ya michezo ya watu wenye ulemavu (Paralimpiki Paris 2024) kupitia mchezo wa mbio za viti-mwendo wa daraja la T54.

Mashindano ya Paralimpiki yanatarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 28 hadi Septemba 8, mwaka huu jijini Paris, Ufaransa.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Chama cha Paralimpiki Tanzania (TPC), Vincent Kaduma, alisema Shawwal amepata fursa hiyo baada ya kuwa mmoja wa washindani bora wa mchezo huo katika mashindano yaliyofanyika hivi karibuni.

Kaduma alisema Hilmy amepata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania katika mashindano hayo ya kimataifa kupitia mchezo wa mbio za viti mwendo baada ya kupokea taarifa za viwango vyake kutoka katika Kamati ya Kimataifa.

"Mchezaji huyu ameshapitishwa na Kamati ya Paralimpiki ya Kimataifa, na sisi tumemtambua kama Mtanzania mwenzetu baada ya kupewa taarifa na kamati hiyo ya Mashindano ya Olimpiki ya Walemavu," alisema Kaduma.

Baba wa Hilmy, Faria Shawwal, aliliambia gazeti hili mtoto wake amekuwa ni mwenye bidii na asiyekata tamaa kwa kushiriki mashindano mbalimbali mpaka alipofanikiwa kupata nafasi hiyo.

"Ni mtoto aliyezaliwa na tatizo la mgongo wazi lakini ni mwenye bidii katika michezo tangu akiwa shule, akiwa darasa la awali alijiunga na michezo mbalimbali hadi kufikia hatua hii ameshapitia mengi na ni matarajio yetu kuwa atashinda" alisema Shawwal.

## Makambo, Yacouba watua rasmi Tabora

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA wa zamani wa Yanga, Heritier Makambo na Yacouba Sogne, wametajwa wako katika hatua za mwisho za kusajiliwa na Tabora United, saa chache kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili hapo jana usiku, imeelezwa.

Habari zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema mastaika hao ni kati ya wachezaji 13 waliokuwa katika hatua za mwisho kusajiliwa na majina yao yalipelekea katika Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

„Watu wamekuwa na wasiwasi kuona tupo kimya, hatujatangaza wachezaji tuliowasajili, tunaowaacha na hata benchi letu la ufundi, kila timu ina utaratibu wake, muda utakapofika tutawatangazia," alisema Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinasema Tabora United ilishindwa kutangaza wachezaji iliowasajili kutokana na kufungiwa na Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA), mpaka itakapomalizana na wachezaji Jean Didie, Ngonyani Junior Mutuale, Danie Chitambai na Makumtima Kisombe, ambao walikuwa wanaidai timu hiyo.

Juzi, TFF ilitangaza kuwafungulia Tabora United baada ya kukamilisha malipo ya wachezaji hao, hivyo ipo huru kusajili.

Mbali na Songne raia wa Burkina Faso aliyeichezea Yanga kuanzia 2020 hadi 2023, na Makambo, aliyeichezea 2019, kabla ya kukimbilia Horoya na kurejea tena 2021 hadi 2023, wengine wanaotajwa kusajiliwa na timu hiyo ya mkoani Tabora United ni Victor Sochima na Chigozie Emmanuel, wote wakitokea Enyimba ya Nigeria.

Nyota wengine ambao watavaa jezi za Tabora United ni Kezie Goodwill na Shedrack Asiegbu, wote wakitokea Rivers United ya Nigeria, Mourice Chikwu na Faria Ondongo (Singida Black Stars), Hiritier Munani (Saint Eloi Lupopo) ya DR Congo, Ismail Mhesa (Mashujaa), Abdallah Seseme (Kagera Sugar), Offen Chikola (Geita Gold) na Nassary Kombe wa Mtibwa Sugar.

Hata hivyo hadi jana mchana, sintofahamu kuhusiana na usajili wa Awesu Awesu, ambaye alitambulishwa katika Tamasha la Simba Day bado ilikuwa haijapatiwa ufumbuzi.

Kamati ya Katiba, Hadhi na Sheria ya TFF iliamua mchezaji huyo anatakiwa kuripoti kwa waajili wake wa zamani, KMC kwa sababu hakufuata kanuni katika kuvunja mkataba wake.

## ZISIKUPITE

### BERGE ATAKIWA UNITED
KLABU ya Manchester United inaweza kumjaribu kiungo wa kati wa Burnley na Timu ya Taifa ya Norway, Sander Berge, mwenye umri wa miaka 26, kwenda Old Trafford kwa kumpa mkataba wa kulipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. ***(Sun)***

### TRIPPER KUTUA WEST HAM
WEST Ham inavutiwa na beki wa kulia wa England, Kieran Trippier, huku mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 huko Newcastle United bado haujaamuliwa. ***(Telegraph)***

### BROJA NJIA PANDA
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Albania, Armando Broja, atafanya mazungumzo na kocha, Enzo Maresca kufahamu mustakabali wake. Everton na Wolves ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

### CHALOBAH ATAJWA WEST HAM
WEST Ham inavutiwa na mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah, mwenye umri wa miaka 26, na beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Mats Hummels (35), ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Borussia Dortmund. ***(Sky Sports)***

### CRSTAL YASAKA MLINZI
KLABU ya Crystal Palace inamtazama mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah, na mlinzi wa Wolfsburg ya Ufaransa, Maxence Lacroix, mwenye umri wa miaka 24, kama chaguo la beki wa kati. ***(Telegraph)***

### CASTEDINE ANUKIA CHELSEA
CHELSEA imewasiliana na Rangers kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa akademi mwenye umri wa miaka 19, Leo Castledine. Aberdeen pia inavutiwa na nyota huyo raia wa England. ***(FootballScotland)***

### BEIER KUTUA LIVERPOOL
LIVERPOOL bado inavutiwa na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani na Hoffenheim, Maximilian Beier, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 anataka kujiunga na Borussia Dortmund na tayari yuko katika mazungumzo na klabu hiyo ya Bundesliga. ***(Sky Germany)***

### SOUTHAMPTON YAWEKA MGOMO
KLABU ya Southampton imepokea ofa kutoka Hoffenheim kwa mlinzi wa miaka 22, Armel Bella-Kotchap. The Saints hao tayari wamekataa ofa ya pauni milioni 8.6 kutoka Stuttgart. ***(Sky Germany)***

### DIGNE AIKATAA GALATASARAY
MLINZI wa Aston Villa, Lucas Digne, amekataa pendekezo la kujiunga na Galatasaray. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 31 anatarajiwa kubaki na Villa. ***(Athletic}***




## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA



# MBAPPE: NIMEANZA RASMI 'KAZI' MADRID

●●●Mshambuliaji huyo asema anaimani atashinda mataji zaidi...

**WARSAW, Poland**

KLYlAN Mbappe amesema „hakuna kikomo" kwa idadi ya mabao ambayo yeye na Real Madrid wanaweza kufunga msimu huu, baada ya kushinda katika mechi yake ya kwanza huku klabu hiyo ikinyanyua UEFA Super Cup kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Atalanta hapo juzi.

Baada ya kipindi kigumu cha kwanza mjini Warsaw nchini Poland, Federico Valverde alianza kufunga dakika ya 59, akiunganisha krosi ya Vinícius Júnior, kabla ya Mbappé kufunga bao lake la kwanza la Madrid dakika tisa baadaye kutokana na shambulizi kali lililowahusisha Rodrygo, Vinícius na Jude Bellingham.

"Tuko Real Madrid, hatuna kikomo, sina kikomo," alisema Mbappé akiiambia Movistar baada ya mechi hiyo alipoulizwa kama mabao 50 ni malengo yake msimu huu.

"Kama naweza kufunga mabao 50, ni 50. Lakini jambo la muhimu zaidi ni kushinda na kuimarika kama timu, kwa sababu tutashinda kama timu."

Mbappé alijiunga na Madrid kwa uhamisho wa bure kutoka Paris Saint Germain msimu huu wa joto, na kusaini mkataba wa miaka mitano na kumaliza sakata la uhamisho wa muda mrefu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alianza mchezo wa Super Cup, ambao uliwakutanisha washindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita Madrid, dhidi ya washindi wa Ligi ya Europa, Atalanta ya Italia, na alicheza kama mshambuliaji wa kati, wiki moja tu baada ya kujiunga na wachezaji wenzake wapya kabla ya msimu.

"Usiku mzuri," alisema Mbappé. „Nimekuwa nikingojea wakati huu kwa muda mrefu, kucheza na jezi hii kwa mashabiki hawa. Ni wakati mzuri kwangu.

"Kushinda kombe ni muhimu sana, tunajua hapa Madrid lazima tushinde. Nina furaha sana, kwa mshambuliaji kama mimi kuwa na maamuzi katika mchezo wangu wa kwanza ni muhimu zaidi."

Madrid iliwapanga Wabrazil Vinícius na Rodrygo pembeni na Mbappé katikati, huku Bellingham akicheza nyuma yake chini ya Kocha, Carlo Ancelotti.

"Ni wachezaji wawili wazuri," alisema Mbappé alipoulizwa kuhusu Vinícius na Bellingham, ambao waliungana kusaidia bao lake.

"Lakini hapa tuna wachezaji bora katika kila nafasi. Nina furaha kucheza na kikosi kizima tulichonacho; tutaimarika kwa hakika, mimi kwanza kabisa, hakika ni hatua nzuri."

Madrid wataanza kutetea ubingwa wao wa LaLiga Jumapili ugenini dhidi ya Mallorca.



# BABA YAKE YAMAL ACHOMWA KISU

**BARCELONA,** HISPANIA

BABA yake nyota wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Lamine Yamal, mwenye umri wa miaka 17 amelazwa hospitalini baada ya kuchomwa kisu katika maegesho ya magari jijini Barcelona, kwa mujibu wa ripoti.

Ikinukuu vyanzo rasmi ambavyo havikutajwa, gazeti la Hispania La Vanguardia na Shirika la Habari la EFE lilisema, Mounir Nasraoui, alichomwa kisu mara nyingi katika kitongoji cha Rocafonda katika mji wa Mataró, kilomita 30 nje ya Jiji la Barcelona.

EFE ilisema Nasraoui alihamishiwa katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Trias i Pujol huko Badalona, Can Ruti, akiwa na majeraha mbalimbali.

La Vanguardia lilisema Nasraoui yuko katika hali mbaya lakini shwari.

Polisi wa Barcelona wameanza uchunguzi kuhusu tukio hilo, ambapo watu kadhaa wanaaminika kushiriki, na tayari baadhi yao wamekamatWa, EFE iliripoti.

Polisi wa eneo hilo hawakujibu mara moja maombi ya maoni kutoka kwa ESPN.

Hispania ilishinda Ubingwa wa Ulaya mnamo Julai na Yamal akiwa sehemu ya timu iliyoshinda.

Alitengeneza bao la ufunguzi la Nico Williams katika ushindi wa 2-1 dhidi ya England na pia alishinda tuzo ya mchezaji bora chipukizi wa mashindano siku moja tu baada ya kufikisha umri wa miaka 17.

# Fernandes ajifunga United

**MANCHESTER,** ENGLAND

BRUNO Fernandes amesema alikuwa na ofa nyingi za kuondoka Manchester United kabla ya kuamua kuongeza mkataba wake na klabu hiyo.

Fernandes ameongeza mkataba wa mwaka mmoja, ambao utamweka Old Trafford hadi 2027, na chaguo la mwaka mwingine.

Lakini kiungo huyo wa kati wa Ureno amefichua kabla ya kufanya uamuzi wa kubaki, kulikuwa na uwezekano wa kuondoka klabuni hapo msimu huu wa joto.

"Kura hii ya imani kutoka kwa klabu ilikuwa muhimu sana kwangu," alisema Fernandes akimwambia Thiago D'Amaral wa ESPN Brasil.

"Hata kwa sababu nilifuatwa na klabu nyingine, klabu ilijua kulikuwa na uwezekano wa mimi kuondoka, nilikuwa na ofa thabiti.



„Lakini klabu ilionesha inanihitaji, ilikuwa wakati wa mabadiliko na walitaka kufanya mambo tofauti."

Mkataba uliopo wa Fernandes, uliokubaliwa Aprili mwaka, 2022, ulipaswa kuisha mnamo 2026.

Akiwa nahodha chini ya kocha, Erik ten Hag msimu uliopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amesema ana matumaini ya kuongeza medali za ushindi wake katika Kombe la FA na Kombe la Ligi kufuatia mabadiliko yaliyofanywa katika muundo wa United chini ya mmiliki mpya, Sir Jim Ratcliffe.

"Ninaamini kuna ndoto ya baadaye katika klabu hii na mabadiliko yanayofanyika," aliongeza Fernandes.

"Ndio maana nilichagua kubaki. Kulikuwa na mwelekeo mwingine ambao ungekuwa wa kuvutia kwangu, matarajio mengine. Lakini ninajisikia vizuri hapa, ninahisi kupendwa na ninahisi kwamba klabu imekuwa ikiniheshimu sana."

Fernandes amekuwa na mafanikio katika United tangu alipowasili kutoka Sporting CP ya Ureno Januari 2020, lakini mafanikio ya timu hiyo yametokana na mashindano ya mataji ya nyumbani.

# Arsenal yakomaa kumsajili Merino

**LONDON,** ENGLAND

ARSENAL na Real Sociedad zinaharakisha mazungumzo juu ya uhamisho wa kiungo wa kati wa Hispania, Mikel Merino, katika klabu hiyo ya Ligi ya LaLiga, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mchezaji huyo, tayari ameshatoa idhini yake kwa hatua hiyo kuendelea. Vyanzo vilisema, lakini makubaliano kati ya klabu bado hayajafikiwa.

Nia ya Arsenal kwa Merino sio jambo jipya. Kocha, Mikel Arteta amekuwa shabiki wa mchezaji huyo kwa muda na anaamini wasifu wake, na mabadiliko katika misimu ya hivi karibuni, ndio timu yake inahitaji.

Merino mwenye umri wa miaka 28, alikuwa sehemu ya kikosi cha Hispania kilichonyanyua taji la Euro 2024, akichangia zaidi kwa ushindi wa muda wa ziada dhidi ya Ujerumani katika robo fainali.

Amekataa mara mbili ofa za kutaka kuongeza mkataba wake na Real Sociedad, na klabu hiyo ya Basque.

Ukubwa wa ada ya uhamisho ndio kikwazo kikuu katika kuhitimisha mpango huo, vyanzo viliiambia ESPN.

Klabu hiyo ya LaLiga inatarajia kupokea angalau euro milioni 35 kwa mmoja wa wachezaji wao nyota, huku Arsenal wakiamini La Real wanaomba kiasi kikubwa mno ikizingatiwa mkataba wa Merino unamalizika 2025.

Hata hivyo, La Real ilikataa ofa ya euro milioni 35 kutoka Atletico Madrid mapema msimu huu wa joto, vyanzo viliongeza. Klabu hizo mbili zina uhusiano mzuri. Hata hivyo, na kuna matumaini kuhusu kufikia suluhu chanya kwa pande zote.



HABARI MICHEZO

# KARIA ATAKA VILABU LIGI KUU KUJIUNGA NA NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia, amevitaka vilabu vinavyoshiriki Ligi Kuu Bara kuwaandikisha wachezaji, makocha na wafanyakazi wao katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kunufaika na mafao mbalimbali yanayotolewa na mfuko huo ikiwamo matibabu.

Karia amesema hayo wakati akifungua semina kwa watendaji wakuu wa timu zinazoshiriki Ligi Kuu, ambayo imeandaliwa na TFF, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPBL) pamoja na NSSF, iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Mafao House Ilala, Dar es Salaam.

Rais huyo alisema zipo faida nyingi za wachezaji na wadau wengine wa mpira kujiunga na kuchangia NSSF ikiwamo kupata mafao pamoja na huduma za matibabu na wategemezi wao na jambo hilo litawasaidia kipindi ambacho hawana nguvu za kucheza mpira.

Amevitaka vilabu vyote kuchangamkia fursa hiyo yenye manufaa kwa wachezaji, na vielekeze nguvu zaidi ya kuandikisha NSSF wachezaji vijana walio chini ya umri wa miaka 20 ili wanapostaafu mpira wanufaike na pensheni ya uzeeni inayotolewa na mfuko huo.

"Tunawashukuru wenzetu wa NSSF kwa kuja na jambo hili kwetu sisi litatuepusha na zile lawama tulizokuwa tunatupiwa ambazo hazituhusu za wachezaji wa zamani kuishi maisha magumu kwa kukosa kukidhi gharama za matibabu na gharama za maisha, angalau sisi tunaosimamia mpira tutahakikisha wachezaji wanaocheza kipindi hiki wasipate changamoto ambazo wanazipata wenzao," alisema Karia.

Naye, Cosmas Sasi, Meneja Uandikishaji, Ukaguzi na Michango wa NSSF, amesema kwa mujibu wa mabadiliko ya sheria ya hifadhi ya jamii sura ya 50 ya mwaka 2018, NSSF ndio Mfuko pekee uliopewa jukumu la kuandikisha wanachama waliopo katika sekta rasmi na sekta isiyo rasmi wakiwamo wachezaji wa soka pamoja na wajasiriamali wengine wote.

"Lengo la NSSF ni kuwafikia wafanyakazi waliopo katika sekta binafsi na tayari kazi hiyo tunaifanya kwa njia mbalimbali, lakini ili kumfikia kila mmoja tuna jukumu la kutoa elimu ya hifadhi ya jamii, mafao tunayotoa na faida zake. Tunashukuru kupata fursa hii ya kujumuika na wenzetu TFF, TPBL pamoja na watendaji wakuu wa vilabu vinavyoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa lengo la kutoa elimu hii ili waweze kujiunga na kuchangia," alisema Sasi.

Aliongeza wachezaji na watendaji wa vilabu vya mpira ni wadau muhimu ambao wanatakiwa wapate kinga ya hifadhi ya jamii ili wanufaike moja kwa moja kipindi ambacho hawana uwezo wa kucheza kwa kupata mafao yatakayowasaidia kuishi maisha bora uzeeni.

"Tutahakikisha elimu ya hifadhi ya jamii inawafikia wana michezo wote hata waliopo vilabu vya chini, lengo wajiunge na kujiwekea akiba kwa ajili ya kesho yao iliyokuwa njema," aliongeza Sasi.

Naye, Meneja wa NSSF Mkoa wa Temeke, Ferouz Mtika, aliishukuru Bodi ya Ligi, TFF na vilabu vya mpira wa miguu kwa kushiriki semina hiyo yenye lengo la kupata elimu ya hifadhi ya jamii.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (katikati waliokaa), akiwa pamoja na maofisa wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Watendaji wa Bodi ya Ligi (TPLB), baada ya kufungua semina ya watendaji wakuu wa vilabu vinavyoshiriki Ligi Kuu Bara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens : Tutawafurahisha

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kutua salama Ethiopia, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amesema wachezaji wake wanajua kilichowapeleka nchini humo na wanafahamu vyema matarajio ya Watanzania.

Simba Queens iko Ethiopia kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa wa Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA), yanayotarajiwa kufanyika kuanzia kesho hadi Agosti 31, mwaka huu.

Mgunda alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanaahidi watapambana kuhakikisha wanatwaa ubingwa wa michuano hiyo.

"Wandele (wasichana) wanajua kilichowafanya waje Ethiopia, licha ya kuwa na jukumu la klabu, lakini wanajukumu la kitaifa, wako vizuri na wako tayari," alisema Mgunda.

Aliongeza kila mechi kwao itakuwa muhimu na hawatawadharau wapinzani wao kuanzia mechi ya kwanza watakaocheza Jumapili dhidi ya FAD kutoka Djibouti.

Simba ambayo imepangwa katika Kundi B itashuka tena dimbani Agosti 20, mwaka huu kuvaana na Kawempe Muslim FC kutoka Uganda na itamaliza mechi za hatua ya makundi dhidi ya mabingwa wa Burundi, PVP Buyenzi siku mbili baadaye.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi mbili za juu zitatinga hatua ya nusu fainali na fainali ya mashindano hayo zitafanyika Agosti 21, mwaka huu.

## Simba mawindoni Bara, Yanga Afrika

INATOKA UK. 24

Fadlu Davis, amebaini moja ya tatizo linalowasumbua baadhi ya wachezaji ni kutokuwa na utimamu wa mwili kwa asilimia 100.

"Kitu ambacho kidogo amekuwa na wasiwasi nacho na ameendelea kukifanyia kazi ni safu ya ushambuliaji na utimamu wa mwili," kilisema chanzo chetu.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi chao kipo imara lakini benchi la ufundi linaendelea kufanyia kazi maeneo yaliyobainika kuwa na mapungufu.

"Mwalimu ameridhishwa na eneo la golikipa, hana mashaka hata kidogo, tulionao anasema wanaweza kuipa Simba mafanikio makubwa, hana wasiwasi na mabeki, hana wasiwasi na mawinga wala viungo, ila anahitaji nguvu tu pale mbele.

Tumepata dakika 180 za wachezaji wetu kucheza, wachezaji wetu wameongeza ufundi na utimamu kwa mwili," Alisema Ahmed.

## Pamba Jiji, Prisons kufungua Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

zamani wa Tabora United.

Naye Mwenyekiti wa Pamba Jiji, Biku Kotecha, aliliambia gazeti hili kila mechi kwao ni muhimu na wamewataka wachezaji kutodharau timu yoyote.

Kotecha alisema wanataka kuanza msimu mpya kwa ushindi na wanaamini wachezaji wao watapata furaha mashabiki wao kwa sababu wanafaida ya kuanzia nyumbani.

Kocha Msaidizi wa Prisons, Shabani Kazumba, alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu timu zote mbili zimejiandaa vizuri.

Kazumba alisema mechi hiyo ni ya ufunguzi, kila mmoja ataiangalia hivyo wachezaji wake wamejiandaa kuonesha kandanda safi.

"Tunakutana na timu ambayo tunaiheshimu, imepambana sana kuhakikisha inapanda daraja," alisema Kazumba.

Aliongeza timu zote 15 zinazoshiriki ligi hiyo wanaziheshimu na wataingia kwa tahadhari kupambana na Pamba Jiji ambayo imerejea na ilikuwa chini ya kocha wao aliyewapandisha ambaye ni Mbwana Makata.

"Tunaenda kukutana na Pamba Jiji, ni timu nzuri, tumewaona walipocheza katika siku ya Pamba Day, tumewasoma, tunajua namna tutakavyowakabili, tutacheza ugenini lakini akili zetu tumepanga kama tuko nyumbani, mwalimu wetu anaijua vizuri Pamba, tunajua tutakavyowakabili," Mussa Mbise, kipa wa Prisons alisema.

Michezo
Ijumaa Agosti 16, 2024
Nipashe

## Mbappe: Nimeanza rasmi 'kazi' Madrid

UKURASA 21



# Simba mawindoni Bara, Yanga Afrika

**Vigogo hao watamba wako vizuri golini ingawa wanahitaji...**



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi ya kuimarisha miili yao kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tabora United itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI vigogo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wakisema wako tayari kuwavaa Vital'O katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. Simba yenyewe imelazimika kuongeza ‚dozi' ili kujiimarisha kwa ajili ya kuwakabili Tabora United.

Simba yenyewe itakuwa katika kampeni ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwakaribisha Tabora United kesho kwenye Uwanja wa KMC Complex ulioko Mwenge, jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jana hawataidharau timu yoyote watakayokutana nayo kwa sababu anaamini hakuna timu dhaifu inayocheza mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kamwe alisema tayari wameshazungumza na wachezaji pamoja na benchi la ufundi na kuwaeleza wanahitaji kupata idadi kubwa ya mabao katika mechi ya kwanza ili kurahisisha kazi kuelekea mchezo unaofuata wa marudiano.

"Ndugu zanguni hakuna timu dhaifu inayocheza Ligi ya Mabingwa Afrika, zote ni ngumu na zote ni mabingwa kwenye nchi zao, kwa hiyo, hatuidharau Vital'O wala hatutakwenda kucheza kwa dharau, tunachohitaji ni kwenda kupambana, ikiwezekana tupate mabao mengi katika mechi ya kwanza ambayo tutacheza Jumamosi, wenzetu wakiwa wenyeji,“ alisema Kamwe.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, aliliambia gazeti hili ameitaka safu ya ulinzi na magolikipa kuongeza umakini huku akiwaongezea mazoezi kwa lengo la kuwaimarisha kabla ya mchezo huo wa kesho.

Gamondi alisema hataki kuona timu yake inakubali nyavu zake kutikiswa kirahisi lakini pia anaitaka safu ya ushambuliaji kutumia kila nafasi itakayopatikana kufunga bao.

„Moja kati ya vitu ambavyo makocha wengi hawapendi ni kuona timu yake inaruhusu mabao kirahisi na kizembe, na tunakwenda kucheza mechi ngumu za kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika, huko michezo ni migumu na watu wanatumia sana makosa madogo madogo kukuadhibu. Tumeanza kulifanyia kazi,“ alisema Gamondi.

Ofisa Habari wa Vital'O, ameonya Yanga isitarajie ushindi kirahisi kwa sababu wao pia wamejipanga kisawasawa kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Wengi wanatuona kama wepesi tu, kwa sababu tumecheza na Pamba Jiji tumetoa sare tena tumesawazisha bao mwishoni, lakini hawajui kila mechi ina mbinu zake, wachezaji wa Pamba ni wazuri, pia hatuwajui kwa sababu hatujawahi kuona video zao, lakini Yanga tunaziona na tunazifanyia kazi,“ alisema.

Yanga na Vital'O zitarudiana Agosti 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na mshindi wa jumla atakutana na kati ya CBE ya Ethiopia au SC Villa ya Uganda.

Wakati huo huo ili kujihakikishia ushindi, wachezaji wa Simba wamerejea kufanya mazoezi ya viungo katika ‚gym', imeelezwa.

Hata hivyo, benchi la ufundi la Simba limesema michezo miwili ya Ngao ya Jamii waliyocheza imewasaidia kuona baadhi ya mapungufu ambayo wameyafanyia kazi.

Taarifa kutoka Simba zinasema Kocha Mkuu,

INAENDELEA UK. 23

# Pamba Jiji, Prisons kufungua Ligi Kuu

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kukaa nje kwa miaka 23, wenyeji Pamba Jiji wanatarajia kuwakaribisha ‚Maafande' wa Prisons kutoka Mbeya katika mechi ya kufungua pazia la msimu mpya wa mwaka 2024/2025 itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Pamba Jiji imerejea baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Ligi ya Championship msimu uliopita, ikiwa nyuma ya mabingwa wa ligi hiyo KenGold ya Mbeya.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Mserbia Goran Copunovic, alisema jana kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu na wataingia uwanjani wakicheza kwa tahadhari.

Copunovic alisema mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu kila timu imejiandaa vizuri na imejipanga kuondoka na matokeo chanya ili kuongeza morali kwa wachezaji wake.

Kocha huyo wa zamani wa Simba alisema wachezaji wake walipata muda mzuri wa kujiandaa na anatarajia watakioneshe kile ambacho wamekifanya wakati wanajiandaa na msimu mpya.

"Nadhani timu imekamilika, kila mmoja amefanya wajibu wake, kilichobaki ni kuonesha kwa vitendo uwanjani,“ alisema kocha huyo wa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >